SUPA JACKPOT
TZS. 1,065,505,647
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**TRIL.** 1/- kujenga upya, kukarabati miundombinu shule za msingi chakavu


Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Ndivyo inavyoshangaza wanahabari kugeuka walimu wabovu Kiswahili
TEKNOLOJIA
NA CHRISTINA MWAKANGALE
ILO yaguswa na kuonya taka za kielektroniki balaa kwa Afrika
• Yataka urejelezaji ili kuzalisha ajira

UKURASA 11

Nipashe
Jumanne Januari 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581186
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Wanafunzi watimuliwa shuleni kisa kutolipa posho mpishi wa shule

**PIA** wamo wanaodaiwa mahindi na maharage. Waziri acharuka, ma-DED matatani... *Endelea ukurasa wa 2*



Mwalimu wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Mdote wilayani Muheza, mkoani Tanga, Fatuma Kiravu (kushoto), akiwafundisha wanafunzi walioanza shule mwaka huu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

UKURASA WA 4

## HOSPITALI KUSHTAKIWA

NDUGU wa mjamzito Rahma Matola, aliyevimba mwili wote baada ya kufanyiwa upasuaji wa tumbo, wanakusudia kuishtaki mahakamani Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo)...

UKURASA WA 7

## WATUMISHI WALIA MANISPAA KUTWAA KITUO CHA AFYA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro imekichukua Kituo cha Afya Moshi/Arusha kilichokuwa kikiendeshwa na sekta binafsi na kukifanya kuwa mali ya umma...



## Fahamu kucha zinavyobeba mwenendo afya ya mwili wako

UKURASA 13

# CHADEMA yasema ruzuku kiporo cha maridhiano

UKURASA 3

MICHEZO MUSONDA, YANGA SASA KIMEELEWEKA UK. 24
KATUNI UK. 6



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu El-Maamry Mwamba (katikati), Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Griffin Mwakapeje (kushoto) na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, wakila kiapo cha maadili kwa viongozi, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Wanafunzi watimuliwa shuleni kisa kutolipa posho ya mpishi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKATI shule zikifunguliwa jana, baadhi ya wazazi wamelalamika watoto wao kurudishwa nyumbani kutokana na kushindwa kupeleka michango, inayojumuisha chakula na fedha kwa ajili ya posho ya mpishi.

Wakizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, wazazi hao walidai kutakiwa kupeleka mahindi debe moja kwa kila mtoto, maharage kilo tano na Sh. 9,000 kwa ajili ya mpishi na mafuta.

Mmoja wa wazazi hao, Daines Msigala, mkazi wa Magegele, Halmashauri ya Mji wa Makambako, alidai kupeleka mtoto wake shuleni, lakini alirudishwa kutokana na kukosa michango hiyo.

"Wanataka chakula shuleni, lakini changamoto kama mimi mwenyewe watoto wa darasa la awali, la kwanza na la pili wote nimetakiwa nitoe michango ya chakula.

"Kama huna chakula, huwezi kupokewa, kama huna mahindi na maharage, huna Sh. 9,000 huwezi kupokewa, mtoto wako unarudi naye nyumbani," alilalamika Msigala.

Alisema tangazo lililotolewa ni kila mwenye mtoto ambaye hajalipa michango arudi nyumbani.

Mzazi mwingine, Asifiwe Mponda alisema wamekwenda shuleni na mwanawe, lakini akaambiwa kama hawana mchango wa chakula warudi na watoto wao nyumbani.

Kutokana na changamoto ya maisha, aliomba wapewe muda ili watafuta michango hiyo," akifafanua: "Bora wangetusikiliza sisi wazazi hata kidogo tutalipa, hawana hata maelewano, tulikaa kikao wakasema kuanzia Januari watoto waje na chakula na fedha, tukakubaliana ila leo tumekwenda wazazi baadhi tulikuwa hatuna hivyo vitu.

"Tumeomba wiki hii tutatoa, hawataki. Kama hujalipa, rudi na mwanao nyumbani kajipigepige utakapopata chakula ndipo uje mwanao atapokewa," alidai Mponda.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, Keneth Haule alipoulizwa na Nipashe kuhusu madai hayo, alisema inawezekana tatizo hilo la watoto kurudishwa nyumbani ni la kweli kwa kuwa amepokea malalamiko ya aina hiyo ofisini.

"Niliongea na mwalimu mkuu asubuhi, alinithibitishia kuwa hilo suala halipo, lakini niliwatuma watu wangu walikwenda huko Magegele na wenyewe walienda kuzikuta hizo changamoto na zoezi la uandikishaji linaendelea.

"Changamoto inaweza kuwa imetokea kwa mzazi mmoja, wawili kwa sababu suala hili la kurudisha watoto limeongewa sana na viongozi na Mkuu wa Mkoa kwenye vikao aliongea na vyombo vya habari vimeongea. Kwa hiyo, unakuta tatizo la mtu mmoja mmoja," alisema.

Hata hivyo, alisema badala ya kuchukua hatua ya kumrudisha mtoto nyumbani, wazazi ndiyo wawajibishwe kwa sababu walikubaliana kwenye vikao, lakini wakashindwa kutekeleza.

"Serikali za mitaa zipo, bodi za shule zipo, kamati za shule zipo wahangaike na mzazi siyo mtoto na nimewaambia kwenye taarifa yangu kwamba mnaposajili watoto na namba za wazazi mnasajili, mpigieni mzazi ikiwezekana mwombe aje shuleni mzungumze naye, siyo suala la kumrudisha mtoto, anahusiana na nini, aachwe aingie darasani," alisema Haule.

Akizungumzia madai hayo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Magegele, Amos Mtawa anayelalamikiwa, alisema suala la chakula linasimamiwa na kamati ya chakula ambayo inachaguliwa na wazazi.

"Utaratibu waliupanga wao kwenye kikao juu ya usimamizi wa ukusanyaji wa chakula. Watoto waliorudishwa siwezi nikalizungumzia maana sijatambua waliorudishwa ni kina nani, ni kosa limefanyika, nitalisimamia," alifafanua Mwalimu Mtawa.

**KAULI YA WAZIRI**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, akizungumzia suala hilo mkoani Kilimanjaro jana, alisema ni marufuku kwa shule za serikali kuchangisha michango kwa lazima.

Prof. Mkenda alisema michango inayoruhusiwa ni ile ya hiari, akitamka: "Serikali imeondoa ada, sasa walimu baada ya kuona ada zimeondolewa, wameweka michango yao kwenye fomu za kujiunga na shule. Kuna watoto wanaacha kwenda shuleni kwa sababu ya hii michango.

"Michango hii ni mingi zaidi ya ile ada tuliyoiondoa. Tunahimiza wazazi wachangie kwa hiari na washirika wachangie lakini hakuna mchango wa lazima.

"Tumeshamwambia Kamishna wa Elimu atoe mwongozo wa kuzuia michango hii, asisitize hizi fomu za kujiunga na shule zinakwenda kinyume cha maelekezo ya serikali kwa kuweka michango ya lazima ambayo ni mingi zaidi kuliko ada iliyofutwa na serikali.

"Unamwambia mtoto ada imefutwa lakini unaweka michango inayofikia laki tatu (300,000/-), tutaanza kufuatilia hizi shule zenye michango hii inayokiuka miongozo, walimu wakuu tutawawajibisha, wakurugenzi wa halmashauri tutamshauri Mheshimiwa Rais waitwe na kujieleza kwanini wanaruhusu hali hii?"

## Samia aapisha Gavana na makatibu wakuu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaapisha Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na makatibu wakuu wawili katika hafla iliyofanyika viwanja vya Ikulu Chamwino, jijini Dodoma jana.

Walioapishwa jana ni Gavana Emmanuel Tutuba aliyechukua nafasi ya Prof. Florens Luoga aliyemaliza muda wake na Dk. Natu El-Maamry Mwamba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, akichukua nafasi ya Tutuba.

Viongozi hao uteuzi wao ulianza Januari 7, mwaka huu.

Aidha, jana Rais Samia alimwapisha Griffin Mwakapeje kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, ambaye uteuzi wake ulitangazwa Januari 5, mwaka huu.

Mwakapeje kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Kisheria kwa Umma, Wizara ya Katiba na Sheria, akichukua nafasi ya Casmir Kyuki aliyemaliza muda wake Januari 7, mwaka huu.

Kabla ya uteuzi huo, Dk. Mwamba alikuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO).

Katika ukurasa wa Twitter wa Ikulu, wananchi waliandika maoni tofauti kuhusu taarifa hiyo ya uteuzi, baadhi wakisema "ajira zinakwenda kwa wenye ajira tayari" na wengine wakidai wanasubiri 'mkeka' wa wakuu wa wilaya. Ally aliandika "Nia yako ni njema kwa taifa lako Mama Samia, Allah azidi kukusimamia na akulinde Rais wetu."

Samson aliandika "Teua mama kazi iendelee, ukiona uliyemwamini haendani na kiapo chake, tengua aende akalime huku watu Ruvuma tunamshukuru Mungu mvua ipo ya kutosha, waje walime ili nchi iwe na chakula cha kutosha."

Aliyejitambulisha kama Mobya, aliandika: "Muwe mnaangalia wahadhiri wa vyuo vingine kwenye uteuzi na siyo Dar es Salaam kila siku, kuna kina MWECAU, Tumaini, MUCCU na KCMC." Naye Charles aliandika: "Tunausubiri mkeka wa ma-DC (wakuu wa wilaya)" huku Mageuzi Mwang'nda akiandika: "Waende kumsaidia Rais kwa nguvu na maarifa makubwa ila Mheshimiwa Rais ombi langu, ukifika kwenye uteuzi za DC tuletee watu kazi maana hata mimi mwenye elimu ya F4 (kidato cha nne) ninashangaa wanashindwa vipi hawa ma-DC kutatua migogoro, wengi wamekaa majigamboni siyo kazi."

Mwombeki Datius aliandika "Nawatakia majukumu mema yaliyo mapya katika utumishi wenu. Taifa tunawategemea sana kuonesha dira na usimamizi mkubwa wa masuala yahusuyo pesa. Tuunge mkono juhudi za Rais Dk. Samia kwa kuliletea maendeleo Taifa."

Wengine waliohudhuria hafla hiyo ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Mpogole na Kamishna wa Maadili Jaji Sivangilwa Mwangesi.

**MWIGULU AMKARIBISHA**

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alimhakikishia Katibu Mkuu mpya na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dk. Mwamba kwamba wafanyakazi wa wizara hiyo watampa ushirikiano wa karibu, ili atekeleze majukumu yake ya kusimamia uchumi wa nchi kwa mafanikio.

Dk. Nchemba alitoa kauli hiyo wakati wa kikao cha kumkaribisha Dk. Mwamba ofisini, akisema: "Karibu sana, uko na timu nzuri, nikuhakikishie kuwa watumishi wote wanafanya kazi kitaalamu na hii ni ishara kwamba ni wabobezi katika majukumu wanayofanya."

Katibu Mkuu mpya na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dk. Mwamba aliushukuru uongozi wa wizara na watumishi kwa kumkaribisha.

Alisema teknolojia inabadilika kila wakati, hivyo aliwashauri watumishi kujenga tabia ya kujiongezea uwezo wa mambo mbalimbali katika kazi zao, ili kuongeza ufanisi na kwenda na wakati.

"Sio kwa mantiki ya kusoma shahada ya uzamili au shahada ya uzamivu, ila kuna zile stadi na vitu kwa kuwa dunia inabadilika kila wakati na kwenda na wakati ni vizuri zaidi," alisema Dk. Mwamba.

## Wanaosadikiwa majambazi wajeruhiwa kwa risasi Dar

**Na Beatrice Moses**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewakamata watu wanne wanaosadikiwa kuwa ni majambazi huku wawili kati yao wakijeruhiwa kwenye majibizano ya risasi na hali zao ni mbaya.

Kamanda wa Kanda Maalum ya Kipolisi, ACP Jumanne Muliro, alisema tukio hilo lilitokea Januari 8, mwaka huu, majira ya saa 6 mchana eneo la Mabibo External, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Alisema watu hao walikuwa na silaha za kivita aina ya AKA 47 yenye risasi 24 waliwashambulia polisi ambao walijibu mashambulizi na kuwapiga risasi wawili na kuwakamata wawili.

Alisema polisi waliwakamata watu hao wakiwatuhumu kujihusisha na vitendo vya kihalifu vya unyang'anyi wa kutumia silaha, kupora pesa katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam na mikoa ya jirani.

Muliro aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni Athuman Mbalilo maarufu kwa jina la Soti (50) Mkazi wa Kimara Temboni na Mpoki Raphael maarufu kwa jina la Mwangwisya (41) mkazi wa Mbezi Luis walipelekwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa matibabu.

Alisema watuhumiwa hao na wenzao wawili ambao hakuwataja majina walikamatwa wakati wakijipanga kutekeleza uhalifu wao na walipobaini kuzingirwa na askari polisi mmoja wao alitoa bastola yake na kufyatua kuwakabili katika mazingira hayo askari nao walijihami na kuwajeruhi na watuhumiwa wote wanne kwa risasi na kufanikiwa kuwakamata.

"Katika kumbukumbu za kihalifu za polisi zimeonesha kuwa miongoni mwao waliwahi kukamatwa na kukaa kwenye mahabusu za Keko kwa tuhuma za mauaji na unyang'anyi na walitoka 2017 na mmoja wao akakimbilia nchi jirani kabla ya kurejea Desemba 2022 na kushiriki matukio kadhaa ya uporaji," alisema Kamanda Muliro

Watu hao wanadaiwa, kupora pesa huku wakitishia bunduki eneo la Kunduchi Mtongani, Goba walitishia silaha na kupora pesa, Keko, na Vikindu Wilaya ya Mkuranga pia walipora pesa, pia kujaribu kupora kwenye duka lililoko eneo la Mtaa wa Tandamti Kariakoo.

"Baada ya kukamatwa waliwaonesha askari bunduki aina ya AK 47 yenye namba za usajili UC 3889 1998 ikiwa na risasi 24 ndani ya Magazine, bastola moja aina Star iliyofutwa namba ikiwa na risasi nne (4) ndani ya magazine na zilikamatwa pia pikipiki mbili aina ya Boxer nyeusi, MC 665 DMD na MC 475," alisema Kamanda.

Aliongeza: "Kutokana na majeraha waliyoyapata wakati askari wakijihami kwa risasi wahalifu hao walipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa matibabu lakini hali zao sio nzuri, juhudi za kuwatafuta majambazi wengine ambao hawajakamatwa zinaendelea na lazima watakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vingine vya kisheria," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linatambua Dar es Salaam ni mji wa kibiashara na uwekezaji na mtaji mkubwa ni suala la usalama na kwamba litaendelea kuimarisha ulinzi.

Baadhi ya wafanyabiashara waliokumbana na vitisho na hatimaye kuporwa fedha zao wamezungumza kwa nyakati tofauti wakithibitisha kutambua pikipiki na begi ambavyo vinatajwa kutumiwa na watuhumiwa hao.

Mmmoja wa wafanyabishara hao Josephat Simamoto alisema kuwa alivamiwa dukani kwake Kunduchi, ambapo kabla ya kumpora walimpiga na kuminya mbavu zake, kisha wakampora fedha na kutoweka wakitumia usafiri wa pikipiki.

"Mmoja alinikaba mwingine akawa anaangalia fedha mle ndani, mimi nilikuwa mbishi kutoa fedha nikapigwa na kitako cha silaha kichwani, nikaminywa mbavu, wakachukua fedha zilikuwa kama milioni tatu," alisema.

Fotnatus Luheneja alisema kuwa walivamiwa kwenye duka lake la shughuli za kifedha lililoko Goba, watu hao walipofyatua risasi, ili kuwatoshia watoe fedha, king'ora cha tahadhari kililizwa na kuzua taharuki katika eneo hilo watu hao walikimbia hivyo hawakufanikiwa kupora.

Luheneja alisema kwa kuwa tukio hilo lilirekodiwa na kamera walipoitwa na polisi wametambua pikipiki, begi hivyo akawashukuru polisi kwa ushirikiano walioutoa.



Meneja mpya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Sospeter Lutonja (katikati), akizungumza jambo na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kulia), wakiwa kwenye ziara ya kukagua na kuzindua miradi ya maji wilayani Mvomero, (kushoto) ni Mbunge wa Mvomero, Jonas Van Zeeland. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# CHADEMA: Ruzuku ni kiporo cha maridhiano

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kitaendelea kutafakari kupokea ruzuku ya serikali au kutopokea kulingana na mazungumzo ya maridhiano baina ya chama hicho, serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), siku za usoni.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, alitoa ufafanuzi huo akizungumza na Nipashe.

"Chama hupata ruzuku ya serikali kutokana na kura za waliogombea ubunge majimboni ambazo hujumlishwa zote na sharti ni kwamba lazima kura hizo zifikie asilimia tano na kuendelea," alisema Mrema.

"Mgawanyo uko hivi, asilimia 50 ya ruzuku inagawanywa kwa idadi ya viti vya ubunge wa majimboni na asilimia 50 inagawanywa kwa idadi ya kura za ubunge mjimboni. CHADEMA sifa ya kupata ruzuku tunayo."

"Tuliambiwa tuna haki ya kupokea ruzuku ya Sh. milioni 102 kwa mwezi, lakini hatujawahi kuipokea mpaka leo. Tutatafakari kadri ya mwenendo wa mazungumzo utakavyokuwa huko mbeleni, kwa sasa sina majibu ya moja kwa moja kwani mazungumzo yanahusu mambo makubwa ya nchi kuliko ruzuku," alifafanua.

Baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba mwaka 2020 chama hicho kilitangaza kususia ruzuku na vyote vinavyopatikana kupitia uchaguzi huo, ikiwamo ubunge wa viti maalum kwa madai hakitambui matokeo na mchakato wake.

Taarifa kutoka ndani ya chama hicho zinaeleza kuwa kutokana na kutokubaliana na uchaguzi huo wa mwaka 2020 pia hakijapeleka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, jina la akaunti ya Baraza la Wadhamini kwa ajili ya kuwekewa fedha hizo za ruzuku.

Kwa mujibu wa taratibu za utoaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa, kila baada ya kumalizika uchaguzi mkuu, Ofisi ya Msajili hukokotoa hesabu ya kura za jumla za kila chama cha siasa kilichoshiriki uchaguzi, ili kupata hesabu kamili ya fedha kwa vyama ambavyo vimekidhi vigezo kutakiwa kupata.

Baada ya mchakato huo, kila chama cha siasa, hujulishwa kiasi kinachopaswa kupokea na kutakiwa kuwasilisha kwa Msajili, jina la akaunti la kupokea fedha hiyo ambayo huwa imefunguliwa na Baraza la Wadhamini na baada ya kupokea fedha hizo, huzipeleka kwenye akaunti ya chama kwa ajili ya kuzitumia kwa maelekezo ya maamuzi ya vikao vyake.

Tayari CHADEMA kinaendelea na mazungumzo ya maridhiano yanayohusisha chama hicho, Serikali na CCM.

Kwa nyakati tofauti CHADEMA, Serikali na CCM wamekuwa katika mazungumzo tangu mwaka jana kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo mchakato wa Katiba mpya, maridhiano ya kisiasa na Tume Huru ya Uchaguzi.

Januari 3, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alikutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini, akatangaza kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa baada ya maridhiano yaliyofanyika mara sita.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mnara wa Tigo wilayani Kalambo, mkoani Rukwa kupitia mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Jumla ya minara mipya 46 nchini imewekwa ikiwa lengo ni kuendelea kujumuisha wananchi wengi zaidi kwenye huduma za kifedha na za kidigitali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Trilioni 1.15/- zatengwa kukarabati shule za msingi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetenga Sh. trilioni 1.15 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi zenye uchakavu kupitia mradi wa kuimarisha elimu ya awali na msingi.

Ukarabati huo unatarajia kuanza kutekelezwa Januari hadi Februali mwaka huu huku baadhi ya shule zitavunjwa na kujengwa upya na nyingine zitafanyiwa ukarabati mkubwa na mdogo ili ziwe na mazingira bora kwa walimu na wanafunzi.

Uamuzi huo wa serikali unajibu hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Aprili 2017, alipofanya ukaguzi maalum wa miundombinu na samani za shule za msingi nchini na kubaini nyingi zina hali mbaya.

CAG, kipindi kile Prof. Mussa Assad, alipendekeza serikali ifanye ukarabati mkubwa na kuzijenga upya baadhi ya shule zenye hali mbaya zaidi kimiundombinu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alibainisha hayo jana alipofungua kikao kazi cha mapitio ya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu kwa mwaka 2022 na mpango mwaka 2023.

Alisema serikali inatambua shule nyingi ni za muda mrefu ambazo zilijengwa na wazee na nyingine kwa njia ya kujitolea na zimedumu kwa muda mrefu na imefika wakati wa kuziboresha shule hizo.

Alisema katika kuendelea kuimarisha Elimu ya Sekondari kupitia mradi SEQUIP, serikali pia imepanga kutumia jumla ya Sh. trilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 1,026 kwenye kata 1,000 na za bweni za wasichana katika mikoa 26 katika kipindi cha miaka mitano.

Waziri huyo alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2021, jumla ya shule 232 za sekondari za kata zimeshajengwa na 10 bweni za wasichana za na za mikoa zinaendelea kukamilishwa ujenzi wake.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2022/23, serikali inategemea kujenga shule mpya za kata 184, moja kila halmashauri na shule tano za bweni za wasichana kwenye mikoa mitano.

Alisema kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, serikali itatoa Sh. milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa shule moja ya sekondari kwa kila halmashauri na zitaangalia maeneo yenye uhitaji.

Akizungumzia hali ya uandikishwaji wa wanafunzi wa darasa la awali na msingi nchini, aliagiza mikoa kuongeza kasi ya kusajili wanafunzi ili kufikia malengo ya asilimia 100 kwa watoto wenye umri wa kuandikishwa.

Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu TAMISEMI, Vicent Kayombo alisema mpango wa kutoa elimu bila ada umeongeza idadi ya wanafunzi wanaosailiwa kujiunga elimu ya awali, msingi na sekondari.

Hata hivyo, alisema kuna dosari kadhaa ikiwamo wanafunzi wanaomaliza darasa la saba bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu huku kukiwa na wanafunzi asilimia 20 wanaoshindwa kufaulu mtihani wa elimu ya msingi na kushindwa kujiunga na kidato cha kwanza na kuwapo idadi ndogo kwa wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kidato cha nne kwa daraja la kwanza hadi tatu.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, alisema wanafunzi walioandikishwa darasa la awali na msingi hadi kufikia tarehe Januari 6, mwaka huu ni 74,578. Kati ya hao, wavulana ni 37,342 na wasichana ni 37,578 sawa na asilimia 94.5.

Alisema miongoni mwa wanafunzi hao ni wenye mahitaji maalum na uandikishaji unaendelea katika shule zote katika mkoa wa Morogoro.

## Hospitali kushtakiwa kisa mjamzito kuvimba

**Na Jumanne Juma**

FAMILIA ya Rahma Matola anayedaiwa kusababishiwa matatizo zaidi ya kiafya baada ya kufanyiwa upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), imesema inafikiria kuchukua hatua za kisheria ili haki ya ndugu yao ipatikane.

Vilevile, imemwomba Waziri wa Afya na Mbunge wa Tanga Mjini, Ummy Mwalimu, kuingilia kati suala hilo kwa kuwa ndugu yao anateseka kwa maumivu huku ankra ya matibabu ikizidi kuongezeka, ikifikia Sh. milioni nne.

Akizungumza na Nipashe jana, Mume wa Rahma, Akida Akida alisema wanajipanga kuchukua hatua za kisheria lakini kwa sasa nguvu kubwa imeelekezwa kwenye kumuuguza mke wake anayeendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Kuhusu maendeleo ya afya ya mgonjwa huyo, alidai anaendelea na matibabu na madaktari watakapojiridhisha kuwa anaweza kuruhusiwa kwenda nyumbani wataondoka naye lakini hawajajua hatima ya ankra ya matibabu.

Akida alidai kutokana na matatizo aliyoyapata Bombo, alipofikishwa Muhimbili, vipimo vinaonyesha amepata tatizo kubwa ambalo awali hakuwa nalo. Akida alitaja maradhi ya mkewe kwa sasa, lakini hatuwezi kuyaweka wazi kutokana na miongozo ya utoaji wa huduma za afya na taarifa za wagonjwa. "Ninaiomba serikali iliangalie suala hili ili kusaidia wengi wanaopata matatizo bila kutarajia kama mke wangu, alikwenda kwa suala la uzazi lakini amesababishiwa matatizo mengine," alidai.

"Inamuuma sana jinsi mke wangu alivyoongezwa maradhi makubwa ya... (anataja ugonjwa) ambayo yanahitaji fedha nyingi za matibabu ambazo hatuna uwezo nazo. Mimi sina kipato kikubwa kutokana na kazi yangu ya kufundisha madrasa," alidai.

Ndugu wa Rahma, Mwasiti Matola alisema ni vizuri serikali ikaingilia kati suala hilo kwa kuwa ndugu yao amesababishiwa matatizo makubwa ya kiafya.

Juzi familia hiyo ililalamikia Hospitali ya Bombo kwa kile ilichodai ni uzembe uliosababisha mgonjwa kufanyiwa upasuaji mara mbili na kumsababishia matatizo zaidi ikiwamo mwili wake wote kuvimba.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga, Naima Zakaria, alithibitisha kupokewa kwa mgonjwa huyo na kufanyiwa upasuaji mara moja na siyo mara mbili kama wanavyodai ndugu zake.

# ...BAVICHA yapongeza maridhiano ya kisiasa, yampa 'tano' Mbowe

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA), limepongeza timu ya viongozi wakuu wa chama hicho ikiongozwa na Mwenyekiti Freeman Mbowe kwa kusimamia vizuri maridhiano baina yao na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwenyekiti wa BAVICHA Taifa, John Pambalu, alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam.

"Tunapongeza timu ya maridhiano ambayo imeongozwa na Mwenyekiti wa chama chetu, Mbowe kwa kipindi cha miezi saba katika mazungumzo na CCM, matunda yameonekana kwa sababu pia sehemu ya wafungwa wa kisiasa wameachiwa huru," alisema Pambalu.

"Katikati ya maridhiano palitokea maneno mengi sana kwamba mwenyekiti wetu sijui 'amelamba asali' lakini ukweli ni kwamba ameonyesha ukomavu na busara ya hali ya juu mpaka kufikia hapa."

Hata hivyo, alisema wanaendelea kuiomba timu ya viongozi wao iendelee na mazungumzo hayo ili muafaka mzuri upatikane katika kila kitu.

"Kikubwa katika maridhiano hayo ni kuona kesi zote za kisiasa zinaondolewa ambazo bado hazijamalizika," alisema Pambalu.

Wanatamani pia kuona kunafikiwa muafaka mzuri wa kupatikana kwa Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi.

**MATUKIO YA 2022**

Alikumbusha baadhi ya matukio yaliyotokea mwaka jana likiwamo la wafanyabiashara ndogo maarufu 'Machinga' kuondolewa maeneo mbalimbali ya mji.

"Katika mwaka ulioisha, wanachinga wengi wameondolewa kwenye maeneo yao waliyokuwa wakiendesha shughuli zao za kiuchumi na hivyo tatizo la ukosefu wa ajira kuzidi kuwa kubwa na vijana wengi wamepoteza mitaji kupitia hili kwa sababu baada ya kuondolewa walipelekwa kwenye maeneo ambayo hakuna uzalishaji kwa sababu hakuna watu," alisema Pambalu.

"Na tatizo hili linasababishwa na serikali yetu kukosa sera ya kushughulikia wafanyabiashara wadogo."

Alisema mwaka 2022 bado vijana wameendelea kupitia magumu ikiwamo kukosa ajira.

"Mwaka 2023 haukuwa rahisi kwetu vijana kwa sababu tumeendelea kukumbana na masahibu makubwa ikiwamo kukosa ajira, licha ya serikali kuahidi ajira, lakini haijaajiri vya kutosha hata sekta binafsi pia nayo imeshindwa kuwaajiri kutokana na kuathirika katika masuala mbalimbali ikiwamo uwekezaji na kodi na taasisi nyingi kulazimika kufunga ofisi zao."

**MAJI, UMEME NA MAFUTA**

Nishati hiyo alisema ni miongoni mwa matukio yaliyochangia kuwarudisha nyuma vijana wengi hususani waliokuwa wakiendesha shughuli za kutegemea maji na umeme.

"Vijana wengi waliokuwa kwenye vituo vya kuoshea magari, saluni walirudi nyuma na wengine walifilisiwa mali zao baada ya kushindwa kulipa mikopo yao kwa sababu walikuwa hawazalishi kwa kukosa maji na umeme," alisema Pambalu.

"Na hata kutumia jenereta ilikuwa ni ngumu kwa sababu gharama ya mafuta ilikuwa juu."

**GHARAMA ZA BANDO**

Alisema gharama ya bando kwa mwaka ulioisha ilikwamisha wengi ikiwamo waliokuwa wakisoma masomo ya moja kwa moja kupitia mitandao.

"Kama hilo halitoshi, athari hii ilienda hata wale wanaoendesha chaneli za mitandaoni, kwa vijana ndio lilikuwa kubwa zaidi kwa sababu ya kipato chao."

**MIKOPO ELIMU YA JUU**

Mwaka 2022, Pumbalu alisema wanafunzi wengi wa elimu ya juu walipata tatizo la kupata mikopo kwa ajili ya kuendelea na elimu ya vyuo vya juu, ikiwamo kutoipata kwa wakati kutokana na vigezo vilivyowekwa.

**MFUMUKO WA BEI**

2022 wananchi wengi walipitia maisha magumu kutokana na vyakula kupanda bei tofauti na ilivyokuwa miaka mingine ya nyuma.

**UELEKEO WAO 2023**

Akizungumzia uelekeo wa Baraza hilo kwa mwaka huu, Pambalu alisema limejipanga kujiimarisha katika vyuo vikuu na vyuo vya kati Bara na Zanzibar, kufanya mfululizo wa mikutano ya hadhara.

Aidha, wataendeleza mchakato wa kudai Katiba mpya mpaka watakapoona muafaka wake, kuongeza usajili wa wanachama pamoja na kuendesha uchaguzi wa ndani kuanzia kwenye matawi.

Wataitumia sera ya vijana taifa kuelezea tatizo la ajira kwa vijana nchini na katika siku ya vijana duniani, Septemba mwaka huu watahakikisha wanaiendesha kwa wiki nzima kuelezea changamoto zinazolikumba kundi hilo.

HABARI KITAIFA

# Korti Kuu yaamuru halmashauri kulipa mamilioni kwa kampuni

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Biashara, Dar es Salaam imeamuru Halmashauri ya Mji wa Tunduma kulipa Kampuni ya Ujenzi ya Mwanakwezi zaidi ya Sh. milioni 100 baada ya kukubali ilikiuka mkataba.

Uamuzi huo ulitolewa mwishoni mwa wiki mbele ya Jaji Dk. Deo Nangela baada ya pande mbili kukubaliana.

Mwanakwezi ilifungua shauri dhidi ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika madai yake aliyowasilisha Septemba 15, 2022, kampuni hiyo iliomba mahakama itoe amri dhidi ya walalamikiwa kwa kukiuka mkataba walioingia.

Aliomba mahakama iamuru alipwe jumla Sh. 171,669,290 (milioni 171.669) kama ilivyo ripoti ya uthamini, malipo ya uharibifu, riba ya asilimia 23 tangu tarehe ya kusitishwa mkataba na tarehe ya kuwasilisha shauri mahakamani.

Pia aliomba alipwe riba ya biashara kiwango cha asilimia 17 kwa mwaka tangu tarehe ya kuwasilisha shauri hadi tarehe ya hukumu, riba asilimia 12 kuanzia tarehe ya hukumu hadi tarehe ya malipo ya jumla. Pia aliiomba mahakama iamuru mlalamikiwa namba moja alipe gharama za kesi na nafuu nyingine ambayo mahakama itaona inafaa.

Katika uamuzi wake, Jaji Nangela alisema kuwa Oktoba 25, mwaka jana, shauri liliitwa baada ya kufika mbele ya mahakama na walalamikiwa waliomba kujibu madai kwa maandishi na walifanya hivyo Novemba 3, mwaka jana.

Alisema kuwa Desemba 8, mwaka jana, Wakili wa mkalamikaji, Daimu Halfani aliieleza mahakama kuwa wahusika wamechagua njia ya usuluhishi nje ya mahakama na Wakili wa Serikali Jaqueline Kinyasi, anayewakilisha walalamikiwa aliunga mkono pendekezo la Wakili Daimu.

Mahakama ilikubali hoja za pande zote mbili na kuunga mkono makubaliano ya kumaliza migogoro nje ya mahakama pale inapowezekana.



"Nilikubali kwa urahisi ombi la wahusika linaloelekeza kwamba iwapo hati yoyote ya suluhu itakuwa iliyokubaliwa iwasilishwe mahakamani mara moja," alisema.

Jaji huyo alisema mawakili wa pande zote mbili Desemba 22 mwaka jana waliifahamisha mahakama kwamba wahusika wamefanikiwa kufanya makubaliano na kwamba wamewasilisha hati ya makubaliano.

Mawakili hao waliomba hati iliyowasilishwa mahakamani irekodiwe kama sehemu ya amri ya mahakama na shauri liwekwe alama ya kusuluhishwa.

"Nimechunguza hati ya suluhu iliyowasilishwa katika mahakama hii kama ilivyoelezwa hapo juu na kuridhika kwamba wahusika wamesuluhisha mzozo wao kwa maelewano juu ya masharti waliyokubaliana chini ya hati yao ya suluhu iliyowasilishwa katika mahakama hii.

"Kwa sababu iliyotajwa hapo juu, mahakama hii inaendelea kutoa amri ifuatayo: Hati ya suluhu inafanywa kuwa sehemu ya hukumu.

"Mlalamikiwa Halmashauri ya Mji Tunduma kwa muda mwafaka anatakiwa kumlipa mkalamikaji Sh. 108,768,978 (milioni 108.769) kwa kumwekea katika akaunti yake," alisema Jaji Nangela.

## Waandishi wa habari wajawa matumaini sheria kurekebishwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDISHI wa habari ambao ni wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), wamesema wanaamini serikali itabadilisha kwa kiasi kikubwa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016.

Wamesema kitendo cha serikali kuahidi kuwasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo kinaonyesha vipengele vilivyokuwa vikilalamikiwa na waandishi wa habari tangu kutungwa kwa sheria hiyo, vitaondolewa na kuwekwa vingine vitakavyoifanya sheria hiyo kuwa imara zaidi.

Waandishi hao waliyasema hayo juzi jijini walipotoa maoni yao kuhusu kauli ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye ya mwishoni mwa mwaka jana kwamba muswada wa kuifumua sheria hiyo utawasilishwa bungeni mwezi huu.

Mwishoni mwa mwaka jana, jijini Dar es Salaam wakati wa Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari, Waziri Nape aliwaambia wadau hao wa habari kwamba serikali imedhamiria kuifanyia marekebisho sheria hiyo na inatarajia kuwasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo wakati wa Bunge la Januari mwaka huu.

"Serikali itafanyia mabadiliko sheria hiyo ya habari kwa wakati na tunatarajia kuwasilisha muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo wakati wa Bunge la Januari mwakani.

"Sisi tunaelewa kwamba, hakuna maendeleo katika nchi yoyote bila kuwa na waandishi wa habari na kwa kulitambua hilo, ndiyo maana tunataka sekta ya habari itumike kuleta maendeleo katika sekta zingine nchini," alisema Nape katika kongamano hilo.

Mmoja wa wajumbe wa DCPC, Arodia Peter, alisema ana matumaini kwamba sheria itakayotungwa baada ya muswada huo kuwasilishwa bungeni, itazingatia maoni ya wadau wa habari waliokuwa wakiipinga na kuikosoa.

"Binafsi sina shaka, ninaamini serikali itatunga sheria bomba kabisa itakayowalinda na kuwaongoza waandishi wa habari katika utekelezaji wa majukumu yao," alisema Arodia.

Fidelis Felix ambaye ni mjumbe wa DCPC, aliishauri serikali isimame kwenye kauli zake kwa kuwasilisha bungeni muswada wa sheria hiyo.

"Ninaamini sheria itakayotungwa itakuwa nzuri, lakini ninachoishauri serikali ni kwamba, ifanye kila inaloweza ili katika Bunge la Januari, iwasilishe bungeni muswada wa sheria hiyo kama Waziri Nape alivyoliambia taifa," alisema.

Naye Janeth Josiah aliungana na wenzake hao kwa kusema ana matuamini na sheria mpya itakayotungwa kwa sababu serikali imeshajua waandishi wa habari wanataka nini kiondolewe katika sheria hiyo na sababu za malalamiko yao walishazieleza.

"Sina hofu kabisa na Bunge letu, ninaamini muswada huo utakapowasilishwa bungeni, wabunge wataujadili kwa kina, mwishowe Tanzania tutakuwa na sheria nzuri ya habari itakayokuwa ikitolewa mfano na mataifa mengine duniani," alisema Josiah.


SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

"Tunayaangaza maisha yako"

**TAARIFA YA KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI NA PIKIPIKI**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linatoa taarifa ya kupotea kwa kadi za magari na pikipiki kama yanavyoonekana kwenye jedwali hapa chini

| S/N | JINA LA CHOMBO CHA USAFIRI | AINA YA CHOMBO CHA USAFIRI | NAMBA YA USAJILI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mitsubishi Pick Up | Gari | SU 33755 |
| 2. | Mitsubishi Pick Up | Gari | SU 35834 |
| 3. | Tata Truck | Gari | SU 33530 |
| 4. | Isuzu NPR | Gari | SU 35940 |
| 5. | Motorcycle Suzuki 125 | Pikipiki | SU 34339 |
| 6. | Motorcycle E-QUINGQI | Pikipiki | SU 36682 |
| 7. | Motorcycle E-QUINGQI | Pikipiki | SU 36683 |
| 8. | Motorcycle E-QUINGQI | Pikipiki | SU 34364 |
| 9. | Motorcycle E-QUINGQI | Pikipiki | SU 36756 |

Kwa yeyote atakayeziona mojawapo ya kadi ya vyombo hivi vya usafiri, tafadhali tunaomba utoe taarifa kupitia anuani ifuatayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO),**
**PLOT 114 BLOCK G DAR ES SALAAM ROAD,**
**S.L.P. 453, DODOMA – TANZANIA.**
**SIMU: +255 748 550 000**
**Barua pepe: communication.manager@tanesco.co.tz**

17220602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri ufuatwe kuepusha madhara kwa wanafunzi

**WAKATI** wanafunzi wakirudi masomoni baada ya shule kufunguliwa ni muhimu maagizo yaliyotolewa na viongozi wa nchi na vyombo vya ulinzi yakafuatwa ili kuepusha yaliyotokea nyuma kwa watoto kufanyiwa ukatili kijinsia na mambo mengine yaliyo kinyume na haki za binadamu, yasijirudie.

Mwaka 2022 matukio mengi mabaya yalijitokeza kwa upande wa wanafunzi na kuwafanya wazazi kuwa katika wakati mgumu wa kuchagua sehemu salama kwa ulinzi wa watoto wao.

Wazazi wengi wanakuwa na amani na kufanyakazi bila wasiwasi, watoto wao wanapokuwa shuleni kwa sababu wanajua ni sehemu salama.

Hata hivyo, matukio yaliyojitokeza kwa baadhi ya shule walimu kuwafanyia ukatili watoto hao waliopewa jukumu na wazazi la kuwalea na kuwafundisha ili waweze kutumiza ndoto za maisha yao, yamewavunja moyo wazazi wengi na wengine kuathirika kisaikolojia.

Mwaka huu 2023 uwe ni wa ulinzi kwa watoto wasiwe waathirika wa matukio hayo ya ukatili ambayo huwafanya baadhi yao kupata athari kisaikolojia.

Wazazi wasikubali kuwaacha watoto wao bila kuwafuatilia kila siku wanaporudi kutoka shule kwa kuwachunguza na kuongea nao ili waweze kuwapa taarifa kama wamefanyiwa vitendo vyovyote vibaya.

Mzazi anapokuwa karibu na mtoto ni rahisi kupata taarifa, lakini anapokuwa mbali na mtoto wake kwa kisingizio cha kazi, atakuja kugundua madhara akiwa amechelewa.

Kuna vitu vingi ambavyo mwanafunzi anahitaji kuwa navyo ili asiweze kuharibiwa ndoto yake ya kufikia malengo aliyojiwekea.

Wazazi wengine wanatamani watoto wao wangepata mahitaji yote ambayo mtoto anatakiwa kuwa nayo awapo shuleni, lakini anashindwa kumtimizia kwasababu ya hali ya kiuchumi.

Watoto wengine hawaelewi hali wanazopitia wazazi wao na wanapoona wenzao wametimiziwa mahitaji yao, wanakuwa na tamaa na kuingia kwenye mtego wa kushawishiwa na watu wasiokuwa na nia nzuri kwao na kuwakatisha masomo.

Juzi Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, aliagiza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza waripoti shuleni hata kama hawana sare za shule.

Hatua hiyo ya Mkuu wa Mkoa ni ya kupongeza kwa sababu wanafunzi wengi wanapoteza fursa walizozipata kwasababu tu ya kukosa sare kutokana na wazazi wao kutokuwa na uwezo wa kununulia.


Ni kweli watoto wanapokuwa na sare zinawatambulisha kuwa ni wanafunzi na vile vile kuleta usawa katika mavazi ili kusiwe na tofauti kati ya mwanafunzi mmoja na mwingine.

Hata hivyo, cha msingi ni elimu atakayopata mtoto anapofundishwa na walimu, bila kujali amevaa vazi la thamani ya kiasi gani.

Vile vile, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwaagiza wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wakurugenzi na maofisa elimu, kusimamia dhamira ya serikali ya kutoa elimu bila malipo kuanzia darasa la elimu ya awali, hadi kidato cha sita kwa kutembelea shule na kukagua fomu za kujiunga na shule na kujiridhisha hakuna michango ya ovyo.

Kadhalika Jeshi la Polisi limewataka madereva wanaoendesha mabasi ya shule wajisimamie badala ya kusimamiwa ili kuhakikisha usalama muda wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Uwepo msukumo kujua Kiswahili, Kiingereza

**BARAZA** la Mitihani (NECTA) hivi karibuni limetangaza matokeo ya mtihani wa darasa la nne na kidato cha pili likieleza kuwa mambo si mazuri kwenye Kiingereza na Kiswahili.

NECTA inaeleza wanafunzi wamedorora kwenye lugha hasa Kiswahili na kimombo, kwa hiyo uelewa wa lugha unaporomoka ikiashiria kuwa hata shule ambazo zinatumia Kiingereza kufundishia tofauti na za umma ufaulu haupendezi.

Zipo sababu nyingi zinazoweza kutajwa kuzungumzia upungufu huo. Wako watakaosema tatizo ni walimu wa Kiswahili na Kiingereza licha ya kwamba Kiswahili kimepigiwa chapuo kuwa lugha ya kimataifa ikiwamo Afrika Kusini kutangaza mkakati wa kukifundisha shuleni na vyuo vikuu, hivyo wengi wanaoina inakubalika zaidi na walitakiwa kuweka msukumo zaidi.

Kadhalika Kiingereza ni lugha ya kimataifa na kwamba zama hizi kina mashiko na kinahitajika zaidi kwa ajili ya kufanyakazi za kikanda na kimataifa.

Aidha, Kiswahili ni muhimu huzungumzwa kwenye mikutano ya Umoja wa Afrika na huenda hata hapa nchini kinapewa kipaumbele zaidi huku Kiingereza kikiendelea kupewa nguvu mpya na hata baadhi ya shule za serikali kuanza shule za msingi zinazofundisha lugha hiyo.

Inawezekana ufundishaji duni na ukosefu wa wataalamu wa kufundisha Kiswahili na Kiingereza kikamilifu unaweza kuwa sababu ya wanafunzi kushindwa lugha hizo.

Kwa upande wa Kiingereza sababu inaweza kuwa ni kukosa wapenzi na wazungumzaji na kusababisha wanafunzi kuichukia na hata kushindwa mitihani kama inavyotokea kwa darasa la nne na kidato cha pili. Lakini, kwa sababu hakuna utafiti uliofanyika kujua kiini na sababu ya watoto kushindwa Kiingereza na Kiswahili na ufaulu duni hakutakuwa na majibu sahihi ya maswali hayo.

Pamoja na changamoto zilizoko ni vizuri kama taifa kukazania wanafunzi kujua zaidi Kiingereza na Kiswahili kuliko zaidi na ikibidi kuwekeza kwenye ufundishaji na matumizi yake kutokana na umuhimu wake kiuchumi, kisayansi na kibiashara duniani.

Kama nchi inayoendelea haiwezekani kupuuza lugha iwe Kiingereza au Kiswahili hili linapaswa kupewa kipaumbele na kuwa na mkubwa na matumizi yake kimataifa, hakuna anayeupinga uhitaji huo kwa kuwa hata katika nchi zilizoendelea ambazo Kiingereza si lugha yao ya asili, bado kinahimizwa na kinatumika.

Ni wazi kuwa hata mataifa yaliyoendelea kiteknolojia, kiuchumi na ugunduzi wa hali ya juu kuanzia tiba, kilimo na uzalishaji viwandani, wanaendelea kutumia Kiingereza ni wazi lugha hiyo ina umuhimu mkubwa na wa kipekee na si ya kupuuza kwa vile imeshakuwa na mizizi katika sekta muhimu duniani za kiuchumi, teknolojia na maendeleo.

Serikali itoke msukumo kwa walimu wa lugha hasa Kiingereza, Kifaransa na hata Kichina pamoja na Kiswahili na kuwalipa vizuri walimu wa lugha hizo ili nchi iwe na watu wanaoelewa lugha.

Kwa mfano kuna maelezo kuwa Japan, Ufaransa, Ubelgiji na Italia mwalimu anayefundisha Kiingereza analipwa vizuri zaidi na hilo ni vyema Tanzania kulitazama ili kuwa na walimu bora wa lugha hapa nchini.

Ukweli ni kwamba Kiswahili kina umuhimu lakini Kiingereza ni lugha ya uwekezaji, biashara, uchumi, teknolojia na kwamba ndiyo inayobeba mawasiliano ya kila mradi wa maendeleo ndani na nje ya nchi na hata kama ni mikataba ya kibiashara, masoko na huduma inafanyika kwa lugha hiyo, si vyema kuipuuza.

Kwa Tanzania ipende isipende Kiingereza ndiyo lugha ya biashara na teknolojia duniani, watu, kampuni za kimataifa zinazungumza Kiingereza na hakuna, biashara au teknolojia masuala ya tiba ya kimataifa bila lugha hii.

Hata magonjwa kama COVID-19, corona, 'hay fever' SARS yote mawasiliano yake ni Kiingereza, hata kama Waswahili watayatafsiri na kusema UVIKO 19, homa ya mgunda, yote hayo ni matokeo ya kukitumia kwanza Kiingereza ili kukifasili kwenye Kiswahili kwa hiyo suala la kutupia macho lugha hizi na kuzifundisha ipasavyo hazina mbadala.

HABARI KITAIFA

## Waziri ateua bosi mpya maji Morogoro

**Na Christina Haule,** ULANGA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amemteua Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Mvomero, Sospeter Lutonja kuwa Meneja wa Mkoa wa Morogoro baada ya kuona juhudi zake katika utekelezaji wa miradi ya maji.

Aweso alitangaza uteuzi huo jana mbele ya viongozi mbalimbali wa chama na serikali, wakiwamo madiwani na mbunge wilayani Ulanga baada ya kuagiza RUWASA makao makuu kumhamishia wilaya nyingine Meneja wa Ulanga RUWASA, David Kaijage kwa kushindwa kusimamia na kuhakikisha miradi ya maji inakamilika kwa wakati.

Waziri Aweso alisema Lutonja anachukua nafasi ya John Msengi ambaye naye amerudishwa makao makuu kupangiwa kazi nyingine baada ya kuonekana kushindwa kusimamia vyema shughuli za utekelezaji miradi ya maji katika mkoa wake.

Alisema kumpandisha Lutonja ni sehemu ya kuonyesha na kuthamini juhudi zake alizofanya katika utekelezaji wa miradi ya maji wilayani Mvomero yenye thamani ya Sh. bilioni tisa, ukiwamo mradi wa maji Tandali- Homboza wenye thamani ya Sh. bilioni 2.9.

Waziri Aweso pia alimpa miezi mitatu Lutonja kusimamia na kuhakikisha miradi ya maji wilayani Ulanga inakamilika kwa wakati na katika kiwango kinachotarajiwa.

"Injinia Lutonja ninakupa miezi mitatu ya kipimo, kama chochote unahitaji, wizara itakusaidia. Ubaki hapa Ulanga, usimamie miradi, uhakikishe inakaa sawa, inakwisha ili uonyeshe juhudi zako ulizofanya Mvomero na watu wa Ulanga wajifunze," aliagiza Aweso.

Akimzungumzia Mhandisi wa Maji Ulanga, Kaijage, Waziri Aweso alisema haiwezekani abaki wilayani humo huku akishindwa kusimamia makandarasi walio chini yake.

Alisema mhandisi ana uwezo wa kumsimamisha kazi mkandarasi kama hana uwezo wa kufanya na kukamilisha kazi na kwamba suala la kumkumbusha na kumwongezea muda halitaleta manufaa yoyote kwa wilaya na taifa kwa ujumla.

"Haiwezekani Ulanga ndiyo iwe kichaka cha wababaishaji, viongozi wanapaswa kusimamia kanuni na sheria za kazi zilizoko katika kutekeleza majukumu yao," alisema.

"Kama kweli mnataka kwenda, lazima tufanye mabadiliko kwenye taasisi na kuanza upya Ulanga na anayekuja, aje afanye kazi shirikishi ili kupiga hatua ya maendeleo kwenye miradi, lazima tupimane kwa kazi.

"Kama sisi tunafanya kazi lazima mtu wa chini naye afanye kazi, asiyefanya kazi tutashughulika naye," alionya Waziri Aweso.

Alisema kuwa katika ziara hiyo, alitegemea wahandisi wangeomba kuongezwa fedha ili kukamilisha miradi badala yake yeye ndiye amekuwa anaibua mambo mengi zaidi yao.

Waziri Aweso alilazimika kukatisha ziara yake ya siku tisa mkoani hapa jana kutokana na kile kilichoelezwa kuwa sababu zilizo nje ya uwezo wake huku akiwa tayari amebadilisha majukumu ya watendaji watano wa RUWASA ili kuleta mabadiliko yenye tija.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo (wa tatu kushoto), akizindua vyumba vya madarasa 12 katika Shule ya Sekondari ya Piki wilayani Wete, Pemba ikiwa ni wiki ya maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Manispaa yakitwaa kituo cha afya

## • Watumishi 26 walia na uamuzi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro imekichukua Kituo cha Afya Moshi/Arusha kilichokuwa kikiendeshwa na sekta binafsi na kukifanya kuwa mali ya umma.

Mabadiliko hayo yanatajwa kuwaathiri watumishi wa kada ya afya, wakiwamo madaktari 26 waliokuwa wakifanya kazi kituoni huko baada ya kukuta zuio la kuingia kituoni.

Jana Nipashe ilifika kituoni huko na kushuhudia watumishi wapya walioko chini ya Manispaa ya Moshi, wakiendelea kufanya kazi hiyo, huku kukiwa na ulinzi wa askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo) kwenye eneo hilo.

Akizungumzia uamuzi huo, Mganga Kiongozi wa Kituo hicho, Dk. Ombeni Mlacha, alisema kuwa tangu serikali ikabidhi kituo hicho kwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi Oktoba 6, mwaka jana, kumekosekana kuelewana miongoni mwa watumishi na hata utaratibu wa matibabu kuvurugwa.

Alisema kuvurugwa kwa utaratibu huo kulianza kuathiri ajira yao, tangu Januari 2, mwaka huu, baada ya manispaa hiyo kupeleka wafanyakazi wapya na kuueleza uongozi kuwa watafanya makabidhiano rasmi kwa maandishi.

Dk. Mlacha alisema kuwa juzi alipokea maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, akimtaka kukabidhi kituo hicho kwa Mganga Kiongozi mpya bila kuwa na maandishi yoyote.

Kutokana na mkanganyiko huo, Dk. Mlacha alisema: "Mimi sikatai kukabidhi kituo cha afya, lakini tambua hapa vipo vifaa mbalimbali. Sasa nitafanyaje makabidhiano bila kuwapo maandishi? Je, kesho na keshokutwa wakija kunigeuka, nitajibu nini mimi? Ninaomba manispaa inipe barua ya kukabidhi ili likija la kutokea, nisije kuulizwa," alisema Dk. Mlacha.

Mganga Kiongozi huyo alisema watumishi wa kituo hicho pia wanadai stahiki zao ikiwamo mishahara ya tangu Januari mwaka jana na hawajui hatima yao.

Alisema kutokana na mgogoro unaofukuta, wanauomba uongozi wa juu serikalini kuingilia kati suala hilo ili walipwe stahiki zao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) Tawi la Moshi/Arusha, Mwanahawa Kitau, alisema serikali ilikuwa katika mchakato wa kuitaifisha hospitali hiyo tangu mwaka 2019.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Rashid Gembe, alisema halmashauri hiyo ilikabidhiwa kituo hicho mwezi Oktoba mwaka jana na Wizara ya Fedha na Mipango.

Alisema kuwa kituo hicho kilikuwa na wafanyakazi waliokuwa wakiendelea kufanya kazi.

Gembe alisema kuwa baada ya kuzungumza na viongozi wa kituo hicho waliokuwa wakifanya kazi, walionyesha wana mkataba uliokuwa unaishia Desemba 31, mwaka jana, hivyo wakaona watumie busara kuwaachia kumaliza mkataba wao ili manispaa ianze kutoa huduma Januari Mosi mwaka huu.

"Tumeshaanza kutoa huduma kwenye kituo hicho kwa kupeleka wafanyakazi wa idara mbalimbali za matibabu, tunafahamu kuwa watumishi waliokuwapo kabla walikuwa na madai mbalimbali ambayo yameshahakikiwa na watalipwa kulingana na taratibu za serikali," alisema Gembe.

**KABWELA** Fadhili Mohamed



# ZRB yatakiwa kuandaa mifumo kielektroniki kukusanya mapato

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, ameutaka Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kuandaa mifumo madhubuti ya kielektroniki itakayosaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi.

Hemed alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa kutathmini utendaji kazi wa ZRB kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Desemba 2022 uliofanyika mjini hapo.

Alisema serikali inahitaji mapato kwa kuendesha miradi ya maendeleo pamoja na kukuza uchumi wake na uwapo wa mifumo madhubuti utasaidia kukuza ukusanyaji huo kwa maslahi ya taifa.

Aliipongeza ZRB kwa mafanikio yanayoendelea kupatikana ambayo ni ya kuridhisha na kusisitiza juhudi zaidi na uwajibikaji wa pamoja unahitajika ili kuimarisha wigo wa ukusanyaji wa mapato.

Alisema watendaji wa ZRB wana wajibu wa kusimamia sheria na taratibu ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Alisema ukusanyaji wa mapato unahitaji nidhamu ya hali ya juu kwa kuheshimu fedha za serikali na kuwataka watendaji hao kuwa waaminifu na wazalendo kwa taifa.

Aliwataka watendaji hao kuwaelimisha na kuwasimamia walipakodi na kuacha muhali ili kulipa kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo alisema serikali inaamini katika dhana ya tozo ndogo kwa walipa kodi ili kila mfanyabiashara na mwananchi alipe kodi kikamilifu.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya Salum, alisema kuwa mafanikio yaliyopatikana katika bodi hiyo yamefikiwa kutokana na maelekezo ya viongozi wakuu wa serikali na kuahidi wataendelea kusimamia maelekezo wanayopatiwa ili kufikia dhamira ya Rais Dk. Hussein Mwinyi ya kujenga Zanzibar mpya.

Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar, Yusuph Juma Mwenda, alisema mkutano huo una lengo la kujitathmini kipindi cha robo mwaka pamoja kuandaa mikakati madhubuti ya kuendeleza bodi hiyo.

Aidha, alisema lengo la ZRB ni kuwa karibu na walipakodi na kufanya suala la ulipaji kuwa rahisi ili kufikia lengo la ukusanyaji.



Taka zilizokusanywa kwenye ufukwe wa bahari jijini Dar es Salaam. **PICHA: HERMAN EMMANUEL- XINHUA**

# Wanawake, vijana wakusanya taka za plastiki fukweni kulinda mazingira

**Na Mwandishi Maalum**

KIKUNDI cha wanawake, vijana wa Tanzania Jumamosi walikusanya tani moja ya taka za plastiki kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi katika Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni hatua ya kuokoa bahari dhidi ya uchafuzi wa mazingira.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Women in Recycling Foundation, Hellen Silas, aliwaongoza wenzake katika kukusanya taka za plastiki kwenye ufukwe wa eneo la Kawe kando ya ufukwe wa Bahari ya Hindi.

"Tuko hapa leo kufanya shughuli za kusafisha fukwe ambazo tumezipanga kwa pamoja na mashirika mengine ya mazingira na watu wa kujitolea kote nchini," Silas aliliambia Shirika la Habari la China, Xinhua katika mahojiano yaliyofanyika baada ya kukamilika kwa shughuli hiyo ya usafi.

Kwa mujibu wa Tovuti ya Gazeti la Umma, China, Silas alisema ukusanyaji wa taka za plastiki kando ya fukwe utafanyika mara moja kila baada ya miezi mitatu. "Suala la kutupa taka za plastiki baharini litakwisha ikiwa tutaendelea kuongeza uelewa na kubadilisha fikra za watu."

Mtetezi wa vijana wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mfuko wa Dharura wa Watoto (UNICEF) katika masuala ya tabianchi, Madina Kimaro, alisema lengo la shughuli hiyo ni kuongeza uelewa kwa watu kuhusu umuhimu wa kulinda mazingira ya maji. "Kwa sababu kadiri tunavyochafua mazingira ya maji, ndivyo maisha ya viumbe wa baharini yanavyokuwa hatarini."

# RC Kunenge atoa somo usimamizi wa mapato

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema endapo usimamizi wa mapato utaimarishwa utaondoa vikwazo vya ukamilishaji wa miradi vinavyotokana na uhaba wa fedha.

Alisema pamoja na mkoa huo kuongoza kwa viwanda, uchangiaji wa Pato la Taifa umebaki kuwa asilimia moja.

Akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya mkoa huo, alisema hali hiyo inatokana na baadhi ya wawekezaji kuendelea kulipa ushuru nje ya mkoa huo na kukosesha mapato Mkoa wa Pwani.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo ambayo alielekeza wawekezaji ambao wanaendelea kulipa ushuru, zilipo ofisi zao kubadilisha utaratibu huo na kuanza kulipa walipowekeza ili mkoa upate mapato na kuongeza uchangiajia wa Pato la Taifa.

Aidha, alizielekeza halmashauri kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo havitakuwa kero kwa wananchi, pia kudhibiti upotevu wa mapato kwa vile vinavyoendelea kukusanya.

Awali, akizungumza kwenye kikao hicho, Ofisa Mipango na Uratibu wa mkoa huo, Rukia Muwango, alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023, mkoa uliidhinisha bajeti ya Sh. 335.110.456.0 kati ya hizo, ruzuku ya matumizi ya kawaida ni Sh. bilioni 206.063.8 na Sh. 80,568.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Sh. 48,478,338,000 za mapato ya ndani ya halmashauri.

Rukia alisema bajeti ya Mkoa wa Pwani kwa mwaka 2022/2023 imeongezeka kwa Sh. 36,279,573,000 sawa na asilimia 12.14 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/2022.

Alisema linatokana na ongezeko la mishahara kwa asilimia 19.38, matumizi mengine (21.82%), fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo (9.44%) na mapato ya ndani ya halmashauri (23.33%).

Pia alisema mkoa huo unakabiliwa na kikwazo cha uchakavu wa vitendea kazi vikiwamo pikipiki na magari.







# Walimu 1,442 wa shule msingi, sekondari wapewa vishikwambi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WALIMU 1,442 wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru wamekabidhiwa vishikwambi ikiwa ni utekelezaji wa serikali katika mchakato wa kurahisisha ufundishaji na kupandisha kiwango cha taaluma shuleni.

Akikabidhi vishikwambi hivyo jana, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, aliwataka walimu kutumia nyenzo hizo muhimu za kidijitali kwa lengo lililokusudiwa ikiwamo kupandisha kiwango cha taaluma shuleni.

"Serikali imeona umuhimu wa walimu kupatiwa vitendea kazi vya kidigitali ili kurahisisha tendo la kufundisha na kujifunzia kwa kuwa walimu wana jukumu la kuvitumia kulingana na maelekezo pamoja na kuvitunza ili kufikia lengo la serikali," alisema Ruyango.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema vishikwambi hivyo vinapaswa kutumiwa kwa mujibu wa miongozo ya serikali kwa kuwa ni mali ya umma na vitasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake.

Alisema mwalimu anatakiwa kutumia vishikwambi kwa ajili ya kupata matini ya masomo, vitabu rejea na video, zinazohusu masomo na siyo vinginevyo.

Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi, Salvatory Alute, alishukuru serikali aliahidi kusimamia matumizi na utunzaji wa vishikwambi hivyo na kuhakikisha vinatumika kupandisha taaluma shuleni. "Tunaamini matumizi ya teknolojia rahisi shuleni yanakwenda kufanya mapinduzi ya kitaaluma kwa kumwezesha mwalimu kupata maarifa na ujuzi ikiwamo mitihani ya masomo, mbinu za kufundishia na kujifunzia kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia,"alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lesiraa, Dora Ngobei, alisema vishikwambi hivyo ni nyenzo muhimu na rahisi itakayomwezesha mwalimu kupata na kuhifadhi matini ya masomo pamoja na vitabu rejea vitakavyomjenga maarifa mapya kila wakati.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Likamba, Richard Mugyabuso alisema: "Hiki ni kitendea kazi muhimu kwa kuwa licha ya kupunguza gharama ya matumizi ya karatasi kitasaidia pia ujazaji wa taarifa kwenye mifumo kwa kuwa awali ilikuwa ngumu kwa shule ambazo hazikuwa na kompyuta."

Vishikwambi hivyo vilikabidhiwa kwa wakuu wa shule za sekondari, walimu wakuu wa shule za msingi pamoja na maofisa elimu wa kata zote kwa niaba ya walimu wote.



Wakazi wa Mji wa Songe, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga wakishiriki kuzima moto katika moja ya nyumba iliyoko Mtaa wa Miembeni. Wananchi hao walilalamika wilaya hiyo kukosa gari la zimamoto na kusababisha athari kubwa kunapotokea majanga ya moto. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Wasindikaji, wachakataji mazao wahimiza kuwatumia wataalamu

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

KAMISHNA Mkuu wa Wakala wa Misitu nchni, Prof. Dosantos Silayo, ameagiza wasindikaji na wachakataji wa mazao ya misitu kuwatumia wataalamu kwa kuwa itasaidia kunufaika na sekta hiyo.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wadau hao jijini Arusha wakati wa kujadili namna ya kuiwezesha sekta hiyo kuchangia ukuaji wa uchumi na pato la taifa.

Alisema licha ya kuwapo kwa ongezeko la viwanda na uuzaji bidhaa za mazao ya misitu nje ya nchi ikiwamo asali na kukua kwa teknolojia ya uchakataji bado kuna umuhimu kwa wadau kuwatumia wataalamu hao.

Prof. Silayo alisema sekta ya misitu bado ina mchango mdogo katika uchumi na pato la taifa kutokana na mambo ambayo yako nje ya uwezo wao.

Alisema wako baadhi ya wauzaji wa bidhaa licha ya kupata masoko ya nje wamekuwa wakiuza bidhaa bora mwanzo lakini baadaye wanapunguza ubora kadiri wanavyoendelea kuzalisha suala ambalo linafanya wateja kuacha kununua.

Kadhalika, alisema kuna tatizo la wawekezaji katika mazao ya misitu kutokuona umuhimu wa kuwa na wataalamu hasa wa hesabu kwenye kazi, hivyo husababisha kuingia kwenye migogoro isiyokuwa ya lazima kati yao na watoza kodi.

"Kuna ongezeko la viwanda na uuzaji bidhaa za misitu nje ya nchi, pia teknolojia ya uchakataji imeongezeka tatizo lililoko ni usimamizi wa ubora asilimia kubwa ya wanunuzi wa wanalalamikia ubora,"alisema Prof. Silayo.

Pamoja na mambo mengine katika mkutano huo walifanya majadiliano yalioongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana akiambatana na wawekezaji.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk.Pindi Chana, aliahidi kuyafanyia kazi matatizo mbalimbali yaliyowasilishwa na wadau hao.

## OSHA yawataka waajiri kuweka mazingira salama kazini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KAIMU Mkurugenzi wa Huduma za Biashara kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Netiwe Mhando, amewaagiza waajiri kuhakikisha wanaweka mazingira salama ya kufanyia kazi ili kuendana na sheria za ndani na kimataifa.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza katika kikao cha majadiliano baina ya Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wa sekta ya utalii.

Alisema OSHA ni miongoni mwa taasisi za serikali zilizoalikwa katika kikao hicho kwa ajili kusikiliza na kutolea ufafanuzi kuhusu matatizo ya wadau yanayohusu utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake.

Alisema katika mkutano wa kimataifa wa masuala ya kazi uliofanyika Juni, 2022 jijini Geneva Uswisi, suala la afya na mazingira salama ya kazi liliainishwa kuwa miongoni mwa haki za msingi za mfanyakazi.

Alisema kutokana na maazimio hayo nchi zote ambazo ni wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), ikiwamo Tanzania zinatekeleza mkataba wa kimataifa namba 155 unaozitaka serikali katika nchi wanachama kuwa na utaratibu na sera ya kitaifa ya usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

Alisema taasisi hiyo imejipanga kushughulikia matatizo yaliyoainishwa na wadau wa sekta ya utalii na sekta nyingine likiwamo suala la ratiba za ukaguzi kutojulikana hivyo kuathiri utoaji huduma.

"Msimu ujao wa ukaguzi wadau wa utalii watakaguliwa kwa wakati mmoja katika kipindi ambacho hakina watalii wengi na hivyo kuwawezesha kukidhi viwango vya usalama bila kuathiri biashara zao," alisema Mhando.

Kaimu Mkurugenzi wa OSHA, Dk. Jerome Materu, alisema taasisi hiyo inafanya jitihada kutekeleza andiko la serikali la uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Alisema miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuondoa tozo zaidi ya 11 zilizoonekana kuwa kero kwa wafanyabiashara na wawekezaji nchini.

Dk. Materu, alisema katika kipindi hiki ambacho watalii wengi wanawasili nchini baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kufanya uhamasishaji kupitia filamu ya The Royal Tour kuna umuhimu wa wadau wa sekta husika kuwekeza katika masuala ya usalama na afya ili kukidhi vigezo vya kimataifa.





# Wachimbaji madini walia bei ghali ununuzi kemikali

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WACHIMBAJI wa madini wameiomba serikali kuingilia kati na kuwachukulia hatua wauzaji wa kemikali ya sodium sanaidi inayotumika kuchenjua madini ya dhahabu kutokana na baadhi yao kufanya udanganyifu kwa kuuza bei tofauti na elekezi.

Wamesema hali hiyo inasababisha wachimbaji wengi hasa wadogo kushindwa kumudu gharama na kuathiri ukuaji wa sekta ya madini.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwa Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko katika kikao cha pili cha wadau wanaojihusisha na uingizaji na usambazaji wa kemikali za kuchenjua madini ya dhahabu kilichofanyika mkoani Mwanza.

Mmoja wa wachimbaji Iddy Mhina ambaye ni Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo mkoani Tanga alisema: "Kemikali ya kuchenjua madini ya dhahabu aina ya 'sodium sanaidi' inauzwa bei ya juu kwa shilingi laki nane kwa dumu moja tofauti na bei iliyoelekezwa na serikali ambayo ni shilingi laki sita kwa dumu.

"Kwa hali hii serikali isipoingilia suala hili kuna uwezekano wa sekta ya madini kuzidi kudorola kimaendeleo".

Rais wa Shirikisho la Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA), John Bina, alisema licha ya kemikali na vifaa vinavyotumika kuchenjua dhahabu kuendelea kupanda bei bado bei ya dhahabu imeendelea kubaki vilevile hali inayoasababisha kazi hiyo kuendelea kuwa ngumu.

Hivyo aliiomba serikali kuweka mkono wake katika kudhibiti bidhaa hizo ili ziwe kama huduma na siyo biashara kwa shushusha viwango vyake vya bei na kudhibiti upandishwaji wa bei holela.

Akieleza mipango ya serikali ya utatuzi wa tatizo hilo, Waziri wa Wadini Dk. Dotto Biteko, alisema serikali imeanza kuchukua hatua kwa wafanyabiashara hao ambao wamekuwa wakitoa risiti yenye bei tofauti na mauzo halisi.

Alisema hatua hiyo ni ukwepaji kodi na kuwadhulumu wachimbaji wadogo wa madini na hivyo kuagiza hatua kali kuchukuliwa kwa wafanyabiashara watatu waliobainika kujihusisha na mchezo huo.

Kuhusu mikakati ya uwezeshwaji na mazingira bora kwa wachimbaji wa madini hasa wadogo, Waziri Biteko alisema serikali itawalinda wachimbaji wadogo na hakuna mfanyabiashara ambaye atajinufaisha kwa kuwaibia.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, wakishuhudia utiaji saini wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya Kibondo-Mabamba Km 47.9, kati ya Mtendaji Mkuu wa TANROADS na Mwakilishi wa Kampuni ya CHICO mkoani Kigoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vyama vya siasa vyashauriwa kutumia mikutano kutatua kero

**Na Waandishi Wetu**

WADAU wa maendeleo mkoani Shinyanga wamevishauri vyama vya siasa kutumia ruksa ya mikutano ya hadhara kwa ajili ya kutatua matatizo ya wananchi.

Pia wametakiwa kutumia mikutano hiyo kuhamasisha maendeleo katika jamii, kuishauri serikali katika harakati za kuinua uchumi wa taifa na mwananchi.

Walitoa maoni hayo mwishoni mwa wiki kwa nyakati tofauti baada ya tamko la Rais Samia Suluhu Hassan kuruhusu mikutano ya hadhara kwa vyama vyote vya siasa.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Tanzania Mzalendo Foundation, Khamis Mgeja alisema wakati wa mkutano hiyo wanatakiwa kujiepusha na lugha za matusi na kuweka nguvu katika kuelezea mazuri yaliyofanywa na serikali pamoja na kunadi sera za vyama vyao na siyo kutumia vibaya ruhusa hiyo kuchafua vyama vingine. Alisema wananchi bado wanayo matatizo yanayowakabili yanayohitaji kusemewa na vyama hivyo ikiwa ni pamoja na kushauri namna ya kuyamaliza ili yaweze kutatuliwa na serikali.

Aidha, alisema kama mwanademokrasia hatua hiyo ni nzuri katika kuimarisha demokrasia ya nchi kwa vitendo na inatakiwa kutumika katika kuhakikisha taifa linakuwa kidemokrasia sambamba na kiuchumi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa alisema: "Tumejipanga vizuri kushindana kwa hoja kwenye mikutano hiyo na hatuna wasiwasi. Alisema zuio la mikutano hata wao liliwaathiri kwa sababu wana mambo mengi ya kuwaeleza wananchi juu ya maendeleo yaliyofanywa na Rais Samia kwa kipindi alichokaa madarakani.

Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Shinyanga akiwamo Ramadhani Kabalo, walisema kurudi kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa itamsaidia Rais Samia katika utendaji wake kazi kwa Watanzania.

**Imeandaliwa na Mohab Dominick (Kahama), Marco Maduhu, (Shinyanga).**

# Diwani achimba bwawa kuhamasisha ufugaji samaki

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

DIWANI wa Kata ya Nyamilangano Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Robert Mihayo, amechimba bwawa kwa ajili ya kuhamasisha ufugaji wa samaki na kilimo cha umwagiliaji cha mboga na matunda kwa vijana walioko katani.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, baada ya uchimbaji wa bwawa hilo, Diwani Mihayo alisema bwawa hilo litakuwa chachu katika kuhamasisha vijana waliohitimu masomo yao na kusalia vijiweni wakisubiria kuajiriwa na atahakikisha anawaunganisha ili kupata mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.

Alisema wakati umefika kwa vijana kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali ili wapate fursa ya kukopeshwa na halmashauri, kutumia fedha hizo katika ufugaji wa samaki na kilimo cha umwagiliaji cha mboga na matunda, kwani kumekuwa na mabadiliko ya tabianchi mara kwa mara na mvua kukosekana.

"Bwawa hili la mfano katika kata yangu ni kwa ajili ya kuhamasisha ufugaji wa samaki na kilimo cha umwagiliaji maji ili kuwafanya vijana kujiajiri na kujiingizia kipato na kuondokana na utegemezi kwenye familia wanazotoka," alisema Mihayo.


Mihayo alisema atashirikiana na maaofisa kilimo na ofisa samaki wa halmashauri katika utoaji wa elimu kwa vijana namna ya ufugaji wa samaki kisasa, kilimo chenye tija, vijana husussani wa kike watapewa kipaumbele na itakuwa sehemu ya kupinga vitendo vya kikatili kwa vijana.

Mkazi wa Kijiji cha Nyamilangano, Alphonce Nyamiti, alisema bwawa hilo litawasaidia kuwapatia elimu ya ufugaji wa samaki na kilimo cha umwagiliaji wa kisasa, watajitokeza kwa wingi kupata elimu ili iwakwamue kwenye maisha na kuondokana na utegemezi katika familia zao.

Naye Matha Maganga alisema msimu huu wa kilimo mvua zimekuwa ndogo kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kwa uwapo wa bwawa hilo litawasaidia kuzalisha zaidi kupitia kilimo cha umwagiliaji na kupata mavuno ya uhakika ya chakula na biashara.

Katika kipindi hiki cha masika katika Wilaya ya Kahama kumekuwa na upungufu mkubwa wa mvua hali ambayo imesababisha mazao mengi kuelekea kukauka na kuleta wasiwasi wakulima wengi katika msimu huu kukosa mavuno ya kutosha.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 10, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


WANENAVYO MALENGA

BABA MBONA UMEJONGO?

Baba mbona umejongo, wapi unapatikana?
Wapi wafanya michongo, vile umeadimika,
Nimetoa hii singo, kwako ipate sikika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Wajua una watoto, lakini umefichika,
Watafuta lako joto, muda limeadimika,
Na zawadi za kitoto, hutumi zikawafika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Mama alivyokuudhi, si sababu kutimka,
Kaa mwombane radhi, watoto wataridhika,
Ni kama wana maradhi, hakuna kuchangamka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Memuachia mkeo, kulea ahangaika,
Mekishusha chako cheo, kichwa kimeadimika,
Familia za wenzao, zenye baba wawacheka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Ninakuambia wewe, ni muda kuwajibika,
Hayo maisha ya mwewe, vifaranga kuvidaka,
Yabaki kwenye vijiwe, watoto wapate cheka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Wanamsifia mama, kwa vile asivyochoka,
Yale malezi mazima, huku yeye apigika,
Baba waweza simama, mkono ukamshika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Kwako mama ni mkate, ingawa alikuchoka,
Na wewe kwake ni mate, hauwezi kuchomoka,
Omba radhi umpate, mkono atakushika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Kwa sababu ya watoto, hebu sasa erevuka,
Acha mambo ya kitoto, mama alishayachoka,
Fanya yale ya mvuto, uweze kukubalika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?


Kama kosa ni ulevi, tangaza umeuchoka,
Uuone kama mavi, huwezi ukautaka,
Kunywa maji hivi hivi, utakako utafika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Ninaisubiri kesho, ili iweze kufika,
Nilipate changamsho, kwa wewe kubadilika,
Uvitoe vichekesho, vile watoto wataka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

Ukurasa 14
WANENAVYO MALENGA


Ukurasa 13
Zifahamu kucha zako kuujua mwenendo wa mwili wako



Ukurasa 12
Ndivyo inavyoshangaza wanahabari kugeuka walimu wabovu Kiswahili

TEKNOLOJIA

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# ILO yaguswa na kuonya taka za kielektroniki balaa kwa Afrika

## • Yataka urejelezaji ili kuzalisha ajira



SHIRIKA la Kazi la Umoja wa Mataifa (ILO), linaonya kuwa ni lazima kuchukua hatua za haraka kudhibiti taka za kielektroniki, huku likiinyooshea kidole Afrika kuwa ni mwathirika namba moja wa shehena ya vifaa vya kielektroniki vinavyotoka ughaibuni.

ILO inashauri kuzirejeleza na kuunda vifaa vingine ikiwa ni njia mojawapo ya kutengeneza ajira kwa mamia ya vijana wanaosaka kuajiriwa au kujiajiri.

Kutokana na zama hizi kuwa za kutumia bidhaa za kielektroniki zikiwamo simu za mkononi, kompyuta, TV, Afrika imekuwa mpokeaji mkubwa zaidi wa vifaa hivyo, vingi vikiwa ni mitumba iliyotumiwa ughaibuni, inasema ILO.

Shehena za 'vifaa taka' hivyo vinatishia usalama wa mazingira, kwa kuwa havidumu, huharibika mapema na kiasi kikubwa kutupwa ovyo majalalani na kusababisha kuchafua mifumo ya maji, ardhi, hewa na kutishia ustawi wa ikolojia.

Shirika hilo linasema kuwa miaka takribani 20 iliyopita nchi tatu pekee Afrika zilitajwa kuongoza kuwa na vifaa kama simu na kompyuta kwa wingi nazo ni Nigeria, Ghana na Afrika Kusini.

Kwa mujibu wa ILO, sasa uwepo wa vifaa vya kielektroniki umesambaa barani na duniani kote.

Taka za kielektroniki zinachafua mazingira kwa kuwa zina viambato vya sumu na madini tembo ( heavy metals kama nikeli) nyingi haziwezi kuoza ardhini, hujilimbikiza katika mazingira hasa kwenye udongo, hewa, maji na ndani ya viumbe hai kama samaki.

Kwa mfano, uchomaji mathalani wa betrii ya simu au kompyuta huchafua hewa, kuongeza asidi ardhini, hewa ukaa angani na kwa ujumla sumu zake zinaingia kwenye mazingira na kuathiri hatima ya viumbe wa ardhini, majini na angani.

**UREJELEZAJI NCHINI**

Angalizo hilo na ILO limeanza kufanyiwa kazi na wataalamu wa masuala ya kielektroniki akiwamo kijana Gibson Kawago.

Mtaalamu huyo anaiambia Nipashe kuwa amebuni utaalamu wa kurejeleza taka za kielektroniki hususan betri za kompyuta kupitia karakana yake anayoiita Wanted Garage-WAGA iliyoko Dar es Salaam.

"Tangu mwaka 2019 nimerejeleza takribani betri 3,100 za kompyuta. Aidha, ninaajiri vijana 32 wakiwamo ambao huokota taka hizo kutoka mikoani na kutoa elimu ya kutunza mazingira kuhusu kurejeleza taka za kielektroniki na wamewafikia watu 3,000." Anasema Kawago.

"Sasa hivi tunazalisha umeme kupitia betri zilizokusanywa kutoka kompyuta zilizokufa na kuchakaa. Tunaufanyia majaribio. Kupitia Shirika la Viwango (TBS) ili kuupitisha na kuruhusu kutumiwa na wateja wengi zaidi," anasema na kuongeza kuwa michakato ya TBS ikiwa tayari wataanza kuwauzia wateja.

Kawago anasema kupitia ubunifu huo, betri hizo hukusanywa na kuzalisha umeme anaoita WAGA Power Pack na huchajiwa na kujaribiwa na baada ya wiki mbili hadi nne, inakuwa kama vile umeme unaozalishwa kiwandani.

"WAGA Power Pack ni betri, yenye uwezo wa volti kuanzia 12, 24 na 48 ambazo zinaweza kutoa mwanga na kutumiwa kama heater ili kuchemsha maji," anasema Kawaga.

Anaeleza kuwa mfumo huo wa uzalishaji umeme unaotumika nyumbani hauzalishi hewa ukaa hivyo hutunza na kulinda mazingira.

Anasema betrii hizo zinaweza kutumiwa kwa saa 13 na kuchajiwa wakati nyingine hutumika kwa mwezi mzima na kuchajiwa baada siku 30.

"Tunajitahidi kubadili maisha na mtazamo wa Watanzania, kutumia vyanzo vya umeme kama hivi."

**WADAU KIMATAIFA**

Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP), linaitaka Afrika kuchukua hatua kukabili ongezeko kubwa la uingizaji wa vifaa vya elektroniki.

Inasema wakati umefika kwa serikali kuwekeza zaidi kwenye mifumo ya kurejeleza na

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA DK. FELICIAN

# Ndivyo inavyoshangaza wanahabari kugeuka walimu wabovu Kiswahili

## • Wanapotosha wakisema, masaa, majumba, wameweza kufariki

NAUNAGANA na wasomaji wa TESA kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuvusha salama mwaka 2022 na kutuingiza 2023 ni zawadi muhimu ya uhai kwa sisi tunaoishi.

Kwa hali hiyo ni wajibu wetu, kufanya kila linalowezekana: kumpenda, kumwabudu, kumtukuza, kumsifu na kumtumikia kwa nguvu zote bila hofu wala kuchoka.

Kama tunavyofahamu Tanzania inaeleweka dunia nzima kuwa lugha yake rasmi ni 'Kiswahili na Kiingereza kinatumika pia.

Lakini Kiswahili ndiyo lugha kuu mijini na vijijini.

Kama umetembelea sehemu mbalimbali vijijini unashuhudia hilo na kusema Mwenyezi Mungu umrehemu hayati Mwalimu Julius Nyerere', Baba wa Taifa, kwa utayari wake na kuhakikisha 'Kiswahili' kinakuwa lugha ya taifa.

Hivyo, kuwezesha makabila zaidi ya 120 nchini, kuwa na lugha patanishi inayozungumzwa na kila kabila. Sasa ni takribani zaidi ya miaka 62 tangu uhuru taifa liko imara na lenye maudhui mazuri na kuelewana bila shida kwa sababu ya uwepo wa Kiswahili, ikiwa ni lugha ya Watanzania wote.

Kwa kuwa Tanzania inatokana na makabila mbalimbali sasa wanaishi wakiwa jamii yenye lugha moja.




Hata hivyo, matamshi kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili yanaendana na lafudhi ya lugha za asili ingawa hicho siyo kikwazo. Changamoto kubwa ni baadhi ya maneno ya Kiswahili kuyatamka kimazoea kutokana na jamii au sehemu anayetamka anapoishi.

Mifano ni kama maneno saa watu wanasema masaa au lisaa, si sahihi, kadhalika taa mataa au litaa, shule hutamkwa mashule; wakati hospitali utasikia mahospitali, kadhalika nyumba wanaita majumba na muda inaitwa mida na dawa pia utasikia madawa.

Maneno yanayoborongwa ni wingi wa neno kama taa au saa. Kawaida kwenye jamii zetu tunayataja vivyo hivyo kimazoea bila wasiwasi kwa hisia kuwa tunatumia Kiswahili sanifu wakati tunakosea.

Kati ya mwaka 1993 na 1994 nikiwa katika tarafa za Nyegezi na Kishapu sasa Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, nilitafiti kuhusu matumizi ya utaalamu wa asili au jadi katika kumudu maisha na kuhifadhi mazingira kwenye vijiji vine vya Nyegezi na Kishapu.

Kwa mwaka mmoja na nusu niliishi wakulima na wafugaji majira yote mvua na kiangazi mwanzoni kwa wafugaji sikupata takwimu sahihi maana nilikuwa na uliza mfugaji una ng'ombe wangapi?

Anajibu nina 'mang'ombe' 20 mwingine 'mang'ombe' 50, wakati ule sikuwa na wasiwasi na Kiswahili sanifu mambo yaliendа hivyo bila kubughudhi watu.

Hata hivyo nilijitahidi nikawa na uhusiano mzuri na wafugaji hivyo nikafanikiwa kupata takwimu zilizoonyesha halihalisi, walikuwapo wenye idadi ya ng'ombe zaidi ya 1,000 hadi 3,000 lakini wote walikuwa wanajibu nina "mang'ombe. Hivyo neno 'mang'ombe' lilitumika kuonyesha wingi wakati wanakosea kutokana na mazoea.

Tanzania inafahamika duniani kuwa waasisi wa lugha ya Kiswahili ni vema watu wakajikita zaidi kwenye Kiswahili sanifu. Pale ambapo hatuna uhakika wingi wa neno husika ni vizuri kuangalia kwenye Kamusi mathalani, 'Kamusi ya Kiswahili Sanifu' ya mwaka 1981 na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Utayarishaji wa kamusi hii ulikusanya na kushirikisha mawazo ya watumiaji na mabingwa wa Kiswahili kutoka karibu kila sehemu inayotumia lugha hiyo.

Miongoni mwao walikuwamo wataalamu wa Kiswahili wanne kutoka Tanga; watatu kutoka Unguja; wawili wakitokea Dar-es-Salaam na mmoja-mmoja Bukoba, Mombasa, Moshi, Musoma na Poland.

Kamusi hii imeweka maneno vizuri na inapobidi wingi wa neno husika umeainishwa laa sivyo neno linabaki vivyo hivyo.

Iwapo ni kwa saa moja au zaidi neno linabaki kuwa 'saa' mfano, kazi ya kufua nguo imenichukua saa moja au saa tano nzima; hakuna sababu ya kusema 'masaa matano mazima'.

Utasikia mwingine akisema 'lisaa lizima' nilikuwa kazini. Utasikia tangazo linatoka hewani "Karibu na 'mataa' ya barabarni" Kiswahili sanifu ni taa za barabarani za kuongoza magari zilizoko eneo fulani badala ya kusema 'mataa au litaa'.

Hivyo hivyo kwa maneno mengine kama shule, hospitali, nyumba, dawa na ndoo.

Katika taaluma ya habari yakiwamo masuala ya utangazaji, uandishi na simulizi mbalimbali yanafanyika makosa, tena kwa kujiamini kuwa kinatumika Kiswahili sanifu wakati sivyo. Ukiacha watangazaji au waandishi pia wapo wanaotumia vyombo vya habari kueleza shughuli wanazofanya wakiwamo viongozi wa kiroho. Neno 'masaa' limezoeleka sana. Kadhalika, unamsikia mtangazaji mzoefu akianzisha kipindi kwa kusema "itatuchukua 'masaa' matatu kukamilisha kipindi". Anapofanya hivyo hajui amekosea Kiswahili wakati ilitakiwa aseme ni 'muda wa saa tatu nzima' badala ya 'masaa'.

Niwaombe waliomo katika tasnia ya habari na utangazaji wajione ni "kioo cha jamii" maana wanatazamwa na usikilizwa na watu wengi ndani na nje ya Tanzania.

Hivyo wajitahidi kuzingatia Kiswahili sanifu kwa faida ya Tanzania na dunia nzima. Watu na watangazaji waachane na "Kiswahili mazoea" maana hakilengi kuimarisha lugha ya taifa kwa ujumla.

Wakosoane palepale ikitokea, kwa bahati mbaya, uliyenaye katika studio ulimi ukateleza akatumia neno lisilo sahihi, asisite kumweleza ili asahihishe.

Matangazo yasanifiwe sawasawa ili maneno yake yazingatie Kiswahili sanifu. Kamusi ya Kiswahili Sanifu iwe ni moja ya vitendea kazi na itumike ipasavyo ili kuboresha na kuimarisha Kiswahili.

Kamusi imefafanua maneno vizuri mfano, 'shamba' limeonyeshwa wingi wake kuwa ni (ma-), lakini neno 'nguo' huwezi kusema 'manguo' linabaki kama lilivyo: 'nguo' moja au 'nguo' nyingi.

Mitaani unaweza kusikia mtu anasema "hebu nipe 'manguo' yangu" bila kujali Kiswahili sanifu. Ikitokea ukasema hivyo ukiwa hewani (studio) rekebisha haraka. Katika kuhabarisha, kutoa matangazo kadhalika katika kuwaburudisha watazamaji na wasikilizaji ni vema Mtangazaji ukawa makini na Kiswahili Sanifu unapokuwa hewani (on-air) kwa faida ya wote.

Vilevile, inapendeza wasikilizaji au watazamaji wanapomsikiliza au kumtazama mtangazaji akisema "asante sana wasikilizaji au watazamaji wetu kwa kuwa pamoja nasi kwa saa 10, Mungu awabariki.

Kuliko kumsikia akisema "...kwa kuwa nasi kwa masaa 19 yaliyopita". Nimalize kwa kuwatakia Watanzania kheri na baraka tele kwa mwaka 2023. Tunaomba uwe mwaka wa kuona Kiswahili sanifu kinatumika zaidi katika vyombo vya habari kwa ujumla wake.

Jambo jingine ni matumizi ya neno ameweza, mfano gari limepinduka na watu 10, wameweza kufariki dunia. Si sahihi acheni kupotosha lugha.

Kumbukeni hakuna lisilowezekana ni uwepo wa dhamira kamili, kuthubutu na kujituma ipasavyo na matokeo chanya yatapatikana.

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Zifahamu kucha zako kuujua mwenendo wa mwili wako

BINADAMU ana viungo kadhaa ambavyo vinaweza kumtambulisha kuhusu afya yake na mojawapo ni ngozi, macho na kucha ambazo zinatambulisha mengi kwa kuzingatia mabadiliko ya rangi.

Tukiangalia macho yakiwa ya bluu tangu kuzaliwa ni utambulisho wa kuwapo na ualbino. Wakati ngozi ikiwa ya njano ni dalili za homa ya jondizi hata matatizo ya ini.

Kadhalika kucha nazo zinaelezea afya yako na kinaweza kuwa kipimo tosha cha kuuchunguza mwenendo wa hali ya mwili, inaripoti makala ya BBC.

Inataja sehemu hii ya mwili kuwa inaweza kuonyesha matatizo mbalimbali ya afya yanayobainishwa na mabadiliko ya rangi, kwenye kucha na vipengele vingine vinavyotumika kama tahadhari kwa magonjwa.

Hii inapotokea, inashauriwa kutafuta daktari wa ngozi ili kutathmini kwa kina na kufanya vipimo kama vile vya damu na daktari anaweza kuamua.

Wakati akishuku kunaweza kuwa na tatizo kubwa mtaalamu wa afya anaweza kuagiza seli au tishu kuchunguzwa zaidi.

Matatizo ya kawaida husababishwa na figo, ngozi, ini, lishe, na hali ambayo mfumo wa kinga ya mwili hushambulia seli zenye afya au autoimmune.

Habari njema ni kwamba tofauti fulani za kucha hazimaanishi shida kubwa kila wakati, mara nyingi husababishwa na utaratibu wa urembo.

"Kucha za miguuni hazitunzwi sana na wakati mwingine zinakabiliwa na matatizo zaidi. Kucha kwa mfano, inaweza kuwa ya njano na nzito," anasema Valéria Zanela Franzon, daktari wa ngozi na profesa wa tiba katika Chuo Kikuu cha Katoliki huko Paraná.



Kucha inaweza kuonyesha upungufu wa damu.



Mabaka haya yanahusishwa na ugonjwa wa ngozi



Ugonjwa wa mycosis unasababishwa na maambukizi ya fangasi au kuvu



Maradhi ya umanjano, figo au saratani ya ini. **PICHA: ZOTE BBC**

### KUASHIRIA MATATIZO

Zifuatazo ni ishara kadhaa ambazo zinaweza kuonyesha matatizo ya kiafya na zinastahili kuchunguzwa:

### KUCHA NYEUPE

Rangi nyeupe, doa jepesi linaweza kuashiria ugonjwa wa mycosis, ni maradhi yanayosababishwa na kuvu au fangasi kwenye ngozi au kucha. Mycosis inaosababishwa na kuambukizwa na vimelea, kama vile upele. Au maradhi yaitwayo psoriasis ambao ni upele kwenye ngozi, lakini wakati mwingine ukihusisha kucha na viungo.

Ugonjwa wa ngozi unaosababisha vipele vinavyowasha, mabaka, magamba, mara nyingi kwenye magoti, viwiko, shina na ngozi ya kichwa na nimonia au homa ya mapafu na hata moyo kushindwa kufanya kazi vizuri.

Ukosefu wa baadhi ya virutubisho, utapiamlo na chakula kukosa protini pia husababisha kuwa na kucha nyeupe.

Aidha kunaweza pia kuonyesha upungufu wa damu pia, husababishwa na ukosefu wa madini ya chuma na kunaweza kufanya ukucha uwe na umbo la kijiko na kukunjamana," asema Juliana Piquet, daktari wa ngozi na mshiriki wa Jumuiya ya Madaktari ya Ngozi ya Brazil na Jumuiya ya Amerika kwa Tiba ya Laza na Upasuaji.

Pia anataja 'leukonychia', ni madoa meupe kwenye kucha, akisema kwa kawaida si ishara ya kutisha, lakini wakati mwingine inaweza kufichua matatizo makubwa ya utaratibu au hali ya kuzaliwa.

Ili kutibu hali hizi, madaktari huwaomba mgonjwa kuchunguza sababu ya tatizo. Kwa hiyo, unashauriwa kufanya vipimo mbalimbali na ufuatiliaji na mtaalamu wa ngozi na wataalamu wengine wa masuala ya moyo na lishe.

### KUCHA YA NJANO

Rangi hii inaweza kuwa na sifa ya urithi wa maumbile au kwa kuzeeka kwa kucha na kuwa nyepesi na kwa rangi ya njano.

Inaweza pia kutokana na rangi inayosababishwa na mycoses au fungasi.

Katika hali mbaya zaidi, pia inaonyesha hali kama vile kuwapo kwa Virusi Vya UKIMWI na ugonjwa wa figo.

Wavutaji sigara wanaweza pia kubadilisha rangi ya kucha zao, kutokana na kushika sigara moja kwa moja. Rangi hii kawaida huonekana kwenye kucha ya kidole kinachoshika sigara.

### MABAKA MEUPE

Mabaka haya yanajulikana kama 'pitting dots' na zinaweza kuonekana kwenye kucha.

Yanahusishwa na ugonjwa wa ngozi unaojulikana kama atopic dermatitis -hali ambayo husababisha ngozi kuwa kavu, kuwasha na kuvimba na hali nyingine za ngozi na nywele.

Ni kawaida kwa watoto wadogo, lakini inaweza kutokea katika umri wowote. Mabaka haya yanahusishwa na ugonjwa wa ngozi unaojulikana kama atopic dermatitis.

### BLUU

Ingawa ni nadra kuwa na kucha za bluu lakini rangi hii inaweza kutokana na matumizi ya dawa maalum. Mojawapo ya kawaida ni zile zinazotibu chunusi na dawa za malaria. Wakati hali hii inapojitokeza, daktari lazima atathmini ikiwa kuna haja ya kusimamisha dawa fulani na kuendelea na aina mpya ya matibabu.

"Inazingatiwa ikiwa kucha ndio udhihirisho pekee na athari ya pili inayokubalika," anaongeza Valéria Zanela Franzon.

Kucha yenye maambukizi ya mara kwa mara ya vimelea fangasi. Ni ugonjwa wa mycosis unasababishwa na maambukizi ya vimelea na unaweza kutokea tena wakati matibabu yanapositishwa.

Kama matibabu hayafanyiki vizuri, vimelea vinaweza kutokea na kushambulia kucha mara kwa mara hata kusababisha kuonekana kama zimekufa au kuoza.

Tatizo linaathiri zaidi kucha miguuni na linapaswa kutibiwa hadi miezi sita.

Katika mikono inashauriwa kutibu kwa muda wa miezi mitatu hadi minne.

Mwathiriwa anapaswa kuzingatia masharti na na wakati unaofaa wa kila dawa na kufuata kwa makini ushauri wa daktari hadi matibabu yatakapokamilika.

### KUWAPO MISTARI

Kitaalamu inajulikana kama mistari ya 'beau', inafanana na mistari ya wima au kulala na inaweza kuonekana baada ya homa kali au matibabu maalum na kuacha kucha zikiwa na makunyanzi zaidi.

Wakati mistari inapokuwa kama meusi au ya kahawia au giza na kuonekana kwenye kidole kimoja tu, inaashiria hali inayofahamika kama melanoma, ambayo ni saratani ya kucha au ya ngozi.

Hata hivyo ukweli unafahamika kwa kwenda hospitalini siyo kuona dalili bila kufanyiwa uchunguzi wa kitaalamu.

# ILO yaguswa na kuonya taka za kielektroniki balaa kwa Afrika

**INATOKA UK.11**



Taka za kielektroniki zinaunda vifaa vingine badala ya kuzitupa ovyo na kuchafua mazingira. **PICHA: MTANDAO**

kuchakata upya taka za kielektroniki kwa kuzingatia kasi kubwa ya ongezeko la taka hizo, takribani tani 50 huzalishwa kila mwaka zikiwa na thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 62.

Ingawa UNEP inatoa angalizo hilo, ni asilimia 20 pekee ya tani hizo za kielektroniki hurejelezwa katika mazingira rasmi.

Kama hiyo haitoshi, mazingira ya kukusanya taka hizo ili zirejelezwe, hawana ujira utokanao na kazi yao, huku wengi wao wakizivunja taka hizo kwa mikono bila vifaa vya kujikinga.

Nikhil Seth ni Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Mashauriano kuhusu kazi zenye utu na taka ngumu, anasema taka za kielektroniki zinazidi kuwa rasilimali muhimu kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na kuongeza mnyororo wa thamani kuanzia kwa wanaoziokota, kuzirejeleza, wabunifu na soko yote yakirahisisha mzunguko wa uchumi.

Seth, anasema lazima kuwapo mfumo bora zaidi wa kusimamia taka hizo kuliko ilivyo hivi sasa.

"Kuhakikisha kuwa taka za kielektroniki zinazozalishwa haziieti madhara. Ikumbukwe ambazo hazijachakatwa zinaweza kuathiri mazingira, afya ya binadamu na wale wanaofanya kazi kwenye viwandani vya taka hizo."

Aidha, ILO na UNEP zinataja umuhimu wa kutumia vijana wenye ubunifu wa kutumia taka za kielektroniki, ikiwa ni fursa na kuongeza nafasi za ajira.

**TCRA**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Septemba mwaka jana, inawahimiza wadau wa vifaa hivyo, kuimarisha ukaguzi wa taka za kielektroniki, kabla ya vifaa hivyo havijaingia nchini, ili kulinda mazingira na janga la taka za kielektroniki.

Meneja wa Usimamizi wa Mawasiliano na Intaneti wa TCRA, Saddath Kalolo, anasema mamlaka hiyo katika kuratibu usimamizi wa taka za kielektroniki, mamlaka ina wajibu wa kuratibu usimamizi vifaa vya kielektroniki vinapofikia mwisho wa matumizi.

"Ili kufanikisha utekelezaji wenye tija katika usimamizi wa taka hizi, TCRA tunashirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira wakiwamo Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC), Tume ya TEHAMA na wadau binafsi wanaohusika na kukusanya taka hizi."

Kalolo anasema mamlaka hiyo, inalo jukumu la kuratibu usimamizi wa taka za kielektroniki kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na taka za kielektroniki umekuwa ukiongezeka kwa kasi na kusababisha athari kwa mazingira.

Anasema uchafuzi wa mazingira utokanao na kutupa ovyo taka za kielektroniki umesababisha Umoja wa Mataifa (UN), kuweka msisitizo wa udhibiti wa utupaji wa taka hizo, kwa kuzingatia miongozo ya Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (ITU).

"TCRA imetoa wito kwa wadau mbalimbali wa mazingira na wananchi kwa ujumla katika kufanikisha utunzaji wa mazingira unaotokana na utupaji sahihi wa taka za kielektroniki."

## WANENAVYO MALENGA

### BABA MBONA UMEJONGO?

Baba mbona umejongo, wapi unapatikana?
Wapi wafanya michongo, vile umeadimika,
Nimetoa hii singo, kwako ipate sikika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Wajua una watoto, lakini umefichika,
Watafuta lako joto, muda limeadimika,
Na zawadi za kitoto, hutumi zikawafika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Mama alivyokuudhi, si sababu kutimka,
Kaa mwombane radhi, watoto wataridhika,
Ni kama wana maradhi, hakuna kuchangamka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Memuachia mkeo, kulea ahangaika,
Mekishusha chako cheo, kichwa kimeadimika,
Familia za wenzao, zenye baba wawacheka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Ninakuambia wewe, ni muda kuwajibika,
Hayo maisha ya mwewe, vifaranga kuvidaka,
Yabaki kwenye vijiwe, watoto wapate cheka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Wanamsifia mama, kwa vile asivyochoka,
Yale malezi mazima, huku yeye apigika,
Baba waweza simama, mkono ukamshika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Kwako mama ni mkate, ingawa alikuchoka,
Na wewe kwake ni mate, hauwezi kuchomoka,
Omba radhi umpate, mkono atakushika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Kwa sababu ya watoto, hebu sasa erevuka,
Acha mambo ya kitoto, mama alishayachoka,
Fanya yale ya mvuto, uweze kukubalika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Kama kosa ni ulevi, tangaza umeuchoka,
Uuone kama mavi, huwezi ukautaka,
Kunywa maji hivi hivi, utakako utafika,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

Ninaisubiri kesho, ili iweze kufika,
Nilipate changamsho, kwa wewe kubadilika,
Uvitoe vichekesho, vile watoto wataka,
Watoto walalamika, mbona baba umejongo?

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Wadau wakutana kupanga mikakati uboreshaji elimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IDARA ya Elimu Mkoa wa Dodoma imefanya kikao kazi cha wadau wa elimu kikiwa na lengo la kujadili mpango kazi na mwelekeo wa namna ya kuanza mikakati ya kuboresha elimu katika mwaka wa masomo 2023.

Mwenyekiti wa kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alibainisha mambo kadhaa katika kikao hicho ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameyafanya na kuboresha kwa kiasi kikubwa sekta ya elimu.

"Rais amefanya mambo mengi kuboresha sekta ya elimu kama vile kuondoa ada kuanzia shule za awali mpaka kidato cha sita, ujenzi wa madarasa ya kutosha kupokea idadi kubwa ya wanafunzi wa kidato cha kwanza.

"Kwa awamu ya kwanza ya fedha za Uviko – 19 mwaka 2021 Mkoa wa Dodoma ulipata fedha za kujenga madarasa 776 na kwa mwaka huu tumepatiwa Sh. bilioni 15.6 kujenga madarasa 339. Pia Rais ametoa ruzuku kwa shule kila mwezi Sh. milioni 200," alisema Senyamule.

Aidha, Senyamule alitoa hamasa kwa walimu kufanya kazi kwa bidii kwani wao ndiyo wanaoweza kusaidia kuinua mkoa katika kupata matokeo mazuri kwenye mitihani ya kitaifa.

Alisema: "Nasisitiza walimu ni kundi linaloweza kujenga nchi au kuibomoa. Nitoe rai kwa maofisa na walimu wakuu kusimamia uandikishwaji wanafunzi wa shule za awali na darasa la kwanza.

"Mpaka sasa wanafunzi walioandikishwa kwa shule za awali wamefikia 57,617 ambapo lengo ni kuandikisha wanafunzi 70,000 na kwa darasa la kwanza wameandikishwa wanafunzi 74,230 sawa na asilimia 82.4 wakati lengo ni kuandikisha wanafunzi 90,122 hivyo uandikishaji haujafikia lengo".

Akizungumzia kuhusu utoro, aliwataka viongozi wote wanaohusika na ufuatiliaji wa wanafunzi kuhakikisha watoto wote watoro wanarudi shuleni.

Alisema: "Hakikisheni wanafunzi wote wanawasili shuleni na tuwahimize wazazi na walezi kuwanunulia wanafunzi mahitaji ya muhimu. Takwimu za utoro kwa Oktoba mwaka jana zilikua wanafunzi 18,883 hivyo nawataka walimu wakuu kuwasilisha ripoti ya utoro kwa watendaji wa kata kila Ijumaa ya wiki."

# Jafo ahimiza utunzaji mazingira kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amewataka wakuu wa mikoa, wilaya, wakuu wa mamlaka za serikali za mitaa na wadau wa mazingira kuunga mkono jitihada za serikali za utunzaji mazingira ili kukabiliana na mabadiliko tabianchi.

Alibainisha hayo jana jijini hapo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushiriki wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwenye maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka huu.

Alisema Rais Dk. Mwinyi mwaka huu amefuta sherehe za maadhimisho hayo kama ambavyo imekuwa ikifanyika kila mwaka na fedha kupelekwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo elimu na afya.

Alisema kutokana na hali hiyo ofisi yake imeandaa ratiba ya matukio mbalimbali ambayo watayafanya katika kipindi hiki cha kuelekea kilele cha maadhimiso ya Sikuku ya Mapinduzi.

"Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Serikali ya Muungano Tanzania tumekuwa tukisherehekea kila mwaka siku hii ya Mapinduzi lakini mwaka huu tutasherehekea kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo upandaji wa miti.

"Wakuu wa mikoa, wilaya na wakuu mamlaka mbalimbali na wadau wa mazingira wanatakiwa kuutumia muda huu wa mvua za masika kupanda miti kwa ajiili ya kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko tabianchi," alisema.

Alisema kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapinduzi Januari 12, leo ofisi yake itaendesha kazi ya upandaji miti katika Barabara ya Dodoma - Morogoro, kuanzia maeneo ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) hadi maeneo ya Kilimo Kwanza.

"Zoezi hili kesho (leo) litaongozwa na mimi mwenyewe waziri mwenye dhamana na muungano na mazingira, lakini Januari 11, litaongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule,"alisema.

Alisema siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapinduzi Januari 12, mwaka huu kazi ya upandaji miti itaongozwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Hata hivyo alisema pamoja na kampeni za upandaji miti zilizoko wananchi wanatakiwa kuhakikisha kuwa miti yote inatunzwa na kukua ili kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko tabianchi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma kuhusu ushiriki wa wizara hiyo katika maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Zanzibar. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Mhadhiri ataka elimu usalama wa chakula kutolewa mara kwa mara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MHADHIRI wa Chuo Kikuu Huria (OUT), Dk. Happy Magoha, amesema elimu kuhusu usalama wa chakula inatakiwa kutolewa mara kwa mara ili kuepuka mazao kupata sumu kuvu na kuepusha madhara kwa jamii.

Aliyasema hayo jana wakati wa semina ya siku tatu inayoendelea jijini Dodoma, huku ukihusisha waandishi wa habari na wahariri kutoka vyombo mbalimbali hapa nchini. Alisema elimu hiyo inatakiwa kutolewa kwa jamii mara kwa mara ili kuhakikisha jamii inatambua umuhimu wa kuhifadhi vizuri mazao ili yasipate sumu kuvu ambayo ina madhara kwa wananchi.

"Wizara ijitahidi kuendelea kutoa elimu kwa jamii tunahitaji kuona jamii inatambua madhara ya sumu kuvu katika mazao," alisema Magoha.

Alisema ndiyo maana wamekuwa wakisisitiza jamii kupatiwa elimu ya namna ya kuepukana na sumu kuvu katika mazao ambayo hutumiwa na binadamu.

Alisema sekta ya habari ni muhimu kutambua suala la sumu kuvu kwa sababu wao hutumika kuelimisha jamii katika mambo mbalimbali hapa nchini.

Kutokana na hilo wameandaa semina ili kuhakikisha wanahabari wanapata uwelewa ili nao wakatoe taarifa kwa watu.

Mratibu wa Mradi wa Sumu kuvu kutoka TAN PAC, Josephat Clepin, alisema sumu kuvu ina malengo makuu matatu kwa jamii, lengo la kwanza ni kuimarisha usalama wa chakula, kuimarisha weledi kwa jamii juu ya sumu kuvu pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ya kujua madhara yatokanayo na sumu kuvu.

Alisema wamekuwa wakijitahidi kuhakikisha elimu hiyo inawafikia walengwa ambao wanahitajika kuelewa madhara ya sumu kuvu ili kuisaidia jamii kutopata matatizo hayo.

Alisema tatizo la sumu kuvu lilianza mwaka 2018 lakini taifa limejitahidi kukabiliana nalo na hadi sasa halipo na kuongeza wanaendelea kutoa elimu ili kuhakikisha jamii inatambua suala hilo.

Alisema semina hii ni moja ya kupanua wigo kwa wahariri na wanahabari juu ya suala la sumu kuvu ambalo linazuilika.



# CST yaombwa kukusanya takwimu za watoto wenye ulemavu nchini

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imeliomba Shirika la kuhudumia Watoto wenye Ulemavu nchini (CST), kukusanya takwimu za watoto hao, kukabidhi kwa serikali ili kupata idadi kamili itayosaidia kutoa huduma stahiki kulingana na mahitaji yaliyoko.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alitoa kauli hiyo juzi kwenye hafla ya kumaliza mradi wa kuboresha mazingira jumuishi na salama kwa watoto nchini.

Chuachua alisema kwa sasa hakuna takwimu sahihi za watoto wenye ulemavu Mkoa wa Mbeya kwa kuwa CST ni wadau wanaoshughulika na masuala ya watoto wenye ulemavu ni vyema wakasaidia kupata idadi kamili ya kundi hilo.

"Kuna tatizo kubwa la takwimu za watoto wenye ulemavu ni kweli kwamba hata ukienda kwenye ofisi za maendeleo huwezi kupata taarifa za watoto hao, tunaomba mtusaidie eneo hili ili serikali iweze kutoa huduma kulingana na mahitaji ya kundi hilo kujua ukubwa wa tatizo," alisema na kuongeza:

Alisema kuna tatizo kubwa la lishe kwa watoto wenye mahitaji maalum hali inayosababisha udumavu na mtindio wa ubongo, aliwaomba wazazi pamoja na walezi kuongeza umakini katika kuwalea watoto.

Alisema licha ya mradi kuboresha mazingira jumuishi na salama kwa watoto nchini kuisha aliliomba Shirika la CST kuendelea kuisaidia serikali kuwaletea na kuwatunza watoto wenye ulemavu. Mkurugenzi wa Shirika la CST, Noela Msuya, alisema watoto 1,000 wenye ulemavu kutoka shule mbalimbali za mikoa ya Mbeya, Rukwa na Dodoma walifikiwa na huduma za kuwasaidia kulingana na hali zao kama vile vifaa visaidizi na mafuta ya kujikinga kwa ajili ya watoto wenye ualbino.

Alisema licha ya kuwasaidia watoto hao lakini wamefanikiwa kuishauri serikali kuhusu sera ya elimu jumuishi ambayo tayari mwongozo uliotolewa, ujenzi na uboreshaji wa elimu kupitia miongozo ambayo inajumuisha upimaji wa watoto.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Mbeya, (SHIVYAWATA), Luca Mahenge, alisema Shirika la CST limesaidia watoto wenye ulemavu kwenda shule.

Alisema kwa sasa tatizo la watoto wenye ulemavu limepungua kwa sababu ya shirika hilo kuhamasisha wazazi kuwapeleka watoto wao shule sambamba na kusaidia mazingira rafiki kwao.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akikagua baadhi ya maeneo ikiwamo Igawilo, Iduda na Iganjo ambayo yaliyoathiriwa na mvua za mafuriko baada ya mvua kubwa kunyesha usiku wa kuamkia Januari 7 mwaka huu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TMA yawaita wanaotaka kutoa utabiri wa hali ya hewa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imewataka wadau wanaotaka kutoa huduma ya utabiri wa hali ya hewa kujisajili ili taarifa wanazotoa ziweze kuthibitishwa na mamlaka hiyo kwani ndiyo yenye jukumu na mamlaka kisheria.

Meneja Huduma za Hali ya Hewa Kilimo nchini, Isack Yona, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hatua zinazopaswa kuzingatiwa kwa wananchi wanaotaka kutoa huduma za hali ya hewa.

Alisema TMA iko tayari kutoa maelezo kwa wananchi, utaratibu unaotakiwa hadi kufikia hatua ya kutoa taarifa za hali ya hewa.

Aliongeza kuwa endapo wakisajiliwa na mamlaka hiyo wahakikishe taarifa zinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuhakikisha vinathibitishwa na kukaguliwa.

"TMA ipo tayari kutoa ufafanuzi kwa wananchi wanaotaka kufahamu taarifa mbalimbali za mamlaka hiyo kwa ajili ya kuwasaidia katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ikiwamo kilimo, jambo la muhimu ni kwa wale wanaotamani kufanya shughuli zetu kuhakikisha wanakuwa na taarifa sahihi kuhusu mamlaka, kujisajili na kufuata kanuni na sheria," alisema Yona.

Alisema TMA iko tayari kutoa ufafanuzi unaohitajika kwa wananchi kuhusu utabiri wa hali ya hewa hususani kwenye shughuli za kilimo.

"Wadudu wengi kwenye mifugo na mimea chanzo chake ni hali ya hewa hata mabadiliko ya mwili wa binadamu pia yanasababishwa na suala hiyo, jambo la muhimu ni kwamba taarifa za hali ya hewa ni muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya taifa kwani zinatoa dira na mwelekeo wa mambo yanayopaswa kufanywa," alisema Yona.

Hivyo aliwaomba wadau mbalimbali nchini kuwekeza kwenye vifaa vya utabiri wa hali ya hewa ili kusaidia upatikanaji wa taarifa maeneo mbalimbali kulingana na mahitaji.

Joseph Ambindwile mkazi kutoka Kata ya Ntaba wilayani Rungwe alisema taarifa alizozipata kuhusu kilimo zimemsaidia kufahamu mambo anayopaswa kufanya kuelekea msimu mpya wa kilimo.

# Mafuriko yasababisha mamia ya wananchi kukosa makazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wakazi wa Kata za Igawilo, Uyole, Iganjo na Iduda wamekosa makazi na mali zao kusombwa na mafuriko baada ya mvua kubwa kunyesha usiku wa kuamkia Januari 7, mwaka huu.

Kutokana na hali hiyo, Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, alifanya ziara ya kuzitembelea kaya zilizoathirika na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha jijini humo.

Katika ziara hiyo Dk. Tulia alijionea athari ya mvua hiyo ikiwamo uharibifu wa miundombinu, nyumba na mali mbalimbali za wananchi katika maeneo hayo.

Dk. Tulia alitoa pole kwa waathirika hao na kuwaahidi kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja jimboni hapo ili kupunguza athari.

Kutokana na athari za mafuriko zilizojitokeza, Dk. Tulia alitoa msaada wa kilo 800 za mchele na kilo 200 za maharage kwa waathirika hao, huku akiahidi kushirikiana na mamlaka za serikali na wadau ili kufanikisha upatikanaji wa misaada zaidi.

"Natoa pole kwa waathirika wote wa mafuriko, najua mmepata hasara kubwa ya samani na nyumba zenu, tupo pamoja katika janga hilo nitawasaidia kwa hali na mali alisema Dk. Tulia.

Aliongeza kuwa tayari amefanya mawasiliano na Waziri Mkuu kuhusu athari zilizojitokeza kwenye mafuriko hayo na kumhakikishia kwamba serikali itakuja kufanya tathmini ili kuona hatua ya kufanya ili kukabiliana na mafuriko.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wakazi wa Igawilo walisema mafuriko hayo yamesomba vitu mbalimbali vilivyokuwa ndani ya nyumba zao na kwamba licha ya madhara hayo lakini athari za kibinadamu zilizojitokeza.

Ambwene Boniface alisema mafuriko hayo yaliingia ndani ya nyumba yake usiku wa kuamkia Januari 7, wakiwa wamelala walishangaa kuona maji yakijaa ndani ya nyumba.

Alisema: "Tunashukuru mbunge wetu amekuja kutusalimia na kutoa misaada mbalimbali hakika tumefarijika eneo letu hili karibu kila mwaka tunapata majanga kama haya, tunaiomba serikali kufanya uchunguzi kujua nini chanzo cha mafuriko haya.".





# Hali ya unywaji maziwa Zanzibar bado inasuasua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Shabani Seif Mwinyi, amesema hali ya unywaji maziwa kwa wananchi wa Zanzibar siyo nzuri.

Amesema hali hiyo huenda ikaleta athari ya kiafya kwa sababu kiwango cha maziwa wanachokunywa kwa mwaka ni kidogo.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa ghala la kuhifadhia chakula na nafaka huko Kizimbani nje ya Mji wa Zanzibar.

Alisema unywaji wa maziwa unakiwango chake ambapo mtu mmoja anatakiwa kunywa lita 200 za maziwa kwa mwaka lakini wananchi waliowengi hawafikii kiwango hicho.

Hivyo, aliwataka wananchi kula chakula kwa kiwango kinachoshauriwa na wataalamu wa afya ikiwamo unywaji wa maziwa kwa sababu kula chakula chini au zaidi ya kiwango ni hatari kwa afya ya binadamu.

Katibu huyo alitaja miongoni mwa athari za kula chakula chini au zaidi ya kiwango ni utapia mlo na udumavu kwa watoto waliochini ya umri wa miaka mitano.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa ghala hilo alisema lengo ni kudhibiti sumu kuvu kwa usalama wa chakula na kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora nchini.

Alisema ghala hilo limejengwa kupitia mradi wa kudhibiti sumu kuvu Tanzania na limegharimu Sh.milioni 630.5 na mradi huo unatekelezwa na Wizara ya Kilimo Bara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ya Zanzibar.

Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, aliwataka wakulima kulitumia ghala hilo kwa ajili ya kuhifadhi mazao yao akisema serikali imeamua kujenga jengo hilo kwa ajili ya wakulima na wananchi.

Aidha, aliwataka wananchi kuacha kujenga nyumba za makazi katika maeneo ya kilimo ili shughuli za kilimo kuendelea na kuwa na chakula cha kutosha.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa ghala hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi, Uwekezaji na Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema chakula ni miongoni mwa mahitaji muhimu kwa binadamu.

Alisema anatambua nafasi na mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa nchi, hivyo ni vyema biashara hiyo kuendelea kuimarika hasa pale wageni watakapopata chakula salama na kutopata madhara yatokanayo na ulaji wa chakula kilicho salama.

Aidha, alisema Wizara ya Kilimo kupitia mradi wa kudhibiti sumu kuvu inaendelea kutoa elimu kwa wadau wote wakiwamo wakulima na wafanyabiashara kuhusu tatizo la sumu kuvu katika chakula na namna ya kudhibiti.

Ghala hilo lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,500 za nafaka ni sehemu ya kuimarisha sekta ya kilimo na afya za wananchi.

## Viongozi, wananchi wahimizwa utunzaji miundombinu

**Na mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema juhudi zinazofanywa na serikali katika uwekezaji wa miundombinu kwenye miradi ya maendeleo lazima viongozi na wananchi waweke mikakati imara ya kuitunza.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la tangi la majisafi na salama eneo la Masinginbi Wilaya ya Magharib 'A' Unguja.

Alisema hatua ya kuwapo kwa miradi ya aina hiyo ni jitihada za Serikali ya Zanzibar kulipa umuhimu mkubwa suala la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa kufanya juhudi mbalimbali ikiwamo uanzishwaji wa miradi mikubwa ya maji ili kuondoa kero kwa wananchi.

Alisema ingawa baadhi ya maeneo bado kuna tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji lakini ukamilishaji wa mradi huo uliohusisha shehia za Masingini, Dole, Dimani, Kwarara Kidutani, Mkorogo, Mfenesini na Maungani itasaidia kupunguza matatizo ya huduma hiyo.

Othman alisema Zanzibar kuna utamaduni wakuwa wazuri wa kuanzisha miradi ya maendeleo lakini tatizo kubwa linabaki katika kuitunza na kuendeleza.

Aidha, aliitaka mamlaka ya maji na viongozi wanaohusika kuhakikisha kwamba wanapanga na kuweka mikakati bora na sera imara za matumizi sahihi ya maji, ili kupunguza tatizo la matumizi makubwa yasiyo ya lazima.

Alisema kwamba eneo la Magharibi ya Zanzibar ndiyo lenye vianzio muhimu vya maji, lakini sehemu kubwa ya maeneo hayo imekatwa miti na kujengwa nyumba.

Amesema hali hiyo itaharibu mazingira na kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi lakini na kukosa ama kuharibika vyanzo vya maji.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Dk. Salha Mohammed Kassim, alisema mradi huo unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Exim ya India kwa masharti nafuu.

Aidha, alisema Sh. bilioni 2.5 zitatumiwa na serikali ili kugharamia ulipaji wa fidia za wananchi ambao mali zao zimeharibiwa kufuatia maeneo yao kupitiwa na mradi huo.



Frateri Denis Msechu (aliyelala madhabahuni) akisimikwa wakfu wa ushemasi kwenye Kanisa la Mtakatifu Joseph mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Maofisa, wapiganaji KVZ kuwekewa mazingira mazuri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali itaendelea kuwawekea mazingira mazuri maofisa na wapiganaji wa idara maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ili waendelee na majukumu yao ya kulinda amani na utulivu nchini.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mradi wa nyumba, mahanga na ofisi za Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ,) kambi ya Muyuni Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni shamrashamra za kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema dhamira ya Mapinduzi Matukufu ya Januari 1964 ni kumkomboa mwananchi mnyonge kwamba serikali inaendeleza dhana hiyo kwa kuwawekea mazingira mazuri kwa kuwapatia miradi ya maendeleo pamoja na nyumba za makazi ya maofisa na wapiganaji.

Makamu huyo alisema ameridhishwa na matumizi mazuri ya fedha zilizotumika katika mradi huo hatua ambayo inaonyesha uimara na uzalendo wa kikosi hicho katika kusimamia fedha za serikali.

"Ni hatua ya kuridhisha kuona kikosi hiki kinaendeleza dhamira ya Mapinduzi kwa kubuni mradi wa kituo cha mafuta, maduka ya kibiashara na mradi wa ufugaji wa kuku wa kisasa katika kambi hii ikiwa ni sehemu ya vyanzo vya mapato,"alisema.

Aidha, alisema mpango huo unaenda sambamba na jitihada za serikali kuzitaka taasisi zote za serikali kubuni vyanzo vya mapato kwa lengo la kujiendesha na kutatua matatizo yanayojitokeza katika uendeshaji wa taasisi.

Hata hivyo, aliwataka maofisa hao na wapiganaji wa KVZ kuthamini juhudi za Rais Dk. Mwinyi kwa kuendelea kuwajibika kwa kufanyakazi kwa bidii na maarifa ili kuendelea kuiweka Zanzibar katika hali ya amani na utulivu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Muhamed, alimpongeza Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kuijenga Zanzibar kimaendeleo na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi katika kambi mbalimbali za idara maalum za SMZ.

Aidha, alisema Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ itaendelea kupokea maelekezo kutoka kwa viongozi wakuu wa nchi yenye lengo la kuimarisha na kukuza idara hizo ili zitekeleze majukumu yao kwa ukamilifu.

Akitoa taarifa ya kitaalamu ya mradi huo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Issa Mahfoudh, alisema utekelezaji wa mradi huo kwa Zanzibar ni wa miaka mitano, kuanzia mwaka 2018 hadi 2023, utagharimu Sh. bilioni 4.170.

Mkuu wa KVZ, Meja Said Ali Juma Shamhuna, alisema majengo hayo yamejengwa katika Kambi ya Muyuni, Kikungwi, Mwanyanya na Mto wa Maji kwa lengo la kuwawekea mazingira mazuri wapiganaji hao pamoja na kuwaweka wananchi katika hali ya usalama.




Mafundi wakiendelea na uwekaji zege kwenye eneo korofi la barabara ya makao makuu ya Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga kuelekea Wilaya ya Gairo Mkoa wa Morogoro jana. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Ukarabati kivuko MV. Kazi watumia bilioni 4/-

**Na Maulid Mmbaga**

KIVUKO cha MV. Kazi kimerejea rasmi katika eneo la Magogoni Kigamboni kwa ajili ya kutoa huduma baada ya kukamilika kwa ukarabati uliogharimu Sh. bilioni 4.4.

Kivuko hicho chenye uwezo wa kubeba abiria 800 na magari 22 sawa na tani 170, kiliondolewa kwenye maji baada ya kufikia muda wake wa ukarabati na kilianza kukarabatiwa Juni 2022, Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), kivuko hicho kimerejeshwa kwenye viwango vinavyotakiwa kimataifa kwa kuzingatia Sheria ya Usalama wa vyombo vya majini inayosimamiwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), ambalo limefanya ukaguzi na kuthibitisha kuwa kivuko ni salama kwa ubebaji wa abiria, magari na mizigo.

"Kukamilika kwa ukarabati wa kivuko cha MV. KAZI kutaboresha huduma za mawasiliano na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali na kuongeza kasi ya maendeleo na ukuaji kiuchumi kwa wananchi.

"Pia kutatoa nafasi kwa kivuko cha MV. Magogoni kwenda kufanyiwa ukarabati baada ya mkandarasi atakayepatiwa jukumu hilo kusaini mkataba baina yake na TEMESA," ilisema.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, serikali ilitoa ahadi ya kuboresha huduma za vivuko nchini ili kuondoa kero za usafiri wa maji wanazopata wananchi maeneo mbalimbali.

Alisema serikali imeanza kutekeleza ahadi hizo kwa kuanza kuvifanyia ukarabati vivuko hivyo na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia TEMESA imedhamiria kutekeleza ahadi hizo kwa kuhakikisha vyote nchini vinakuwa vya uhakika na salama kwa matumizi ya wananchi.

Aidha, TEMESA iliahidi kuwa vivuko vitakarabati na kununuliwa vipya katika maeneo yote ya nchi yanayohitaji vivuko kadri uwezo wa bajeti ya serikali utakavyoruhusu na inatekeleza ahadi hizo kwa kulenga dhamira ya serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Ukarabati wa kivuko cha MV. Kazi umehusisha kufunga injini mpya nne, matengenezo makubwa ya (Propulsion Units), ukarabati wa milango, kubadilisha mabati yaliyochakaa na kuweka mapya, kupiga rangi umbo la kivuko, kuweka mabomba mapya ya maji na mafuta.

"Mengine ni kufunga taa mpya za kisasa, vipaza sauti, televisheni mpya pamoja na vifaa vipya vya kisasa vya kuongozea kivuko, vifaa vya tahadhari na uokoaji, vinavyoendana na viwango vinavyotakiwa kimataifa," ilisema.

Vile vile, TEMESA iliishukuru serikali kwa kuiwezesha kifedha katika utekelezaji wa mradi huo na kuahidi kufanya kazi kwa weledi na jitihada ili kufikia malengo na matarajio.

## WAJIKI yataka jitihada kukabili rushwa ngono

**Na Halfani Chusi**

TAASISI ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), imesema katika kukabiliana na vitendo vya rushwa ya ngono, wenye mamlaka wananafasi kubwa kumaliza tatizo hilo.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Janeth Mawinza, akiongea jijini Dar es Salaam jana kwenye mkutano wa wazazi wa Kata ya Makumbusho, aliwataka wazazi kuwa walinzi namba moja kwa watoto.

Alisema mkutano huo umewakutanisha na wazazi, ambao ni watoa uamuzi kwenye ngazi ya familia na wakipewa elimu ya malezi na wakaelewa kwa kina kuna uwezekano mkubwa wa kutokomeza vitendo hivyo.

"Tumelazimika kupenyeza ujumbe wetu kwa wazazi kupitia mkutano huu, lengo ni kupata saini zaidi ya 1,000 za watakao kuwa mstari wa mbele kulinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili na kukemea rushwa ya ngono.

"Baada ya hapo saini hizo tutazipeleka kwa Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla, ambaye ndiye kinara wa mapambano dhidi ya vitendo hivyo," alibainisha na kuongeza:

"Wazazi wana nafasi kubwa ya kuwaepusha watoto dhidi ya vitendo visivyofaa kwenye jamii, mzazi anapaswa kuwa mtu wa kwanza kugundua iwapo mtoto amefanyiwa ukatili."

Musa Mpangwa, miongoni mwa wazazi waliohudhuria mkutano huo, alisema ukatili kwa watoto unatokana na baadhi ya wazazi kutotimiza wajibu wao vizuri kwenye malezi.

"Watoto wanakumbwa na ukatili wa kijinsia kwa sababu wazazi hatuchezi kwenye nafasi zetu ipasavyo, mtoto inabidi anaporudi shule mzazi umwite ukae naye, akague madaftari yake na kumuuliza kwa ujumla alivyoshinda shuleni kwa siku hiyo," alisema.

Monika Juma, aliiomba serikali na wadau wengine wa maendeleo kuungana na taasisi hiyo ili kufanikisha safari ya mtoto wa kike akibainisha kuwa elimu waliyopewa imebadili mtazamo wao.

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**AFRICAN JACK INVESTMENT CO.LTD**

inatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 627 CHQ**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa **IRI/IRI/RB/8153/2023.**

**KUPOTEA KWA KADI YA CHETI**



17220202

**ALOYCE J FULANA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **NS0744/0079** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya NANGA mwaka **2015,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Polisi taarifa DAR/URA/RB/11567/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA CHETI**



17220102

**BRIGHTON PIUS NYAMBACHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S2365-0014** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ANDREW FAZA MEMORIAL SEKONDARY** mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Control No. 9910835485581.**

**MWAMBA MILLENNIUM COMPANY LIMITED**

**TANGAZO TANGAZO MNADA WA HADHARA**

Kwa Niaba ya MWALUKO RAPHAEL NDEJEBI Tutaendesha mnada wa hadhara wa kuuza vitu mbalimbali vilivyoko katika Nyumba yake kikuyu Dodoma Mjini, Mnada utafanyika tarehe 18.01.2023 saa tano kamili asubuhi (05:00)

**MASHARTI YA MNADA**

- Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
- Mnunuzi atalipa 100% bei itakayowekwa kwenye mnada.
- Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki yake.
- Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu namba **0712245977, 0684364501, 0756364501**

**WOTE MNAKARIBISHWA**

Adrian Mpiluka
Mkurugenzi

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT
REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**DEED POLL**



The documents presented for registration on the **30-12-2022** at **1:00PM** herewith the original of the above mentioned documents registration having under folio/s **2018** and serial/s **03/2023** knowledge receipt of the enclosures here to.

**URES:**

**SIGNED AND DELIVERED BY SAID WERIMA WEGORO KAGWEGULA**
Who is known to me personally
Identified to me by....the letter being known to me personally.
This **30** day of **12 / 2022.**

DEPONENT

**BEFOR ME:**

BEFORE ME
Name
Signature
Postal Address
Date
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

# Siku tatu za maombolezo Senegal

**DAKAR, Senegal**

RAIS wa Senegal, Macky Sall, ametangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa, baada ya vifo vya watu 39 vilivyotokana na ajali iliyohusisha mabasi mawili ya abiria.

Katika hotuba yake kwa taifa, aliyoitoa jana Rais Sall, alisema katika ajali hiyo zaidi ya watu 100 walijeruhiwa, huku akiziagiza mamlaka husika kuwachukulia hatua madereva wazembe.

Rais Sall, alisisitiza kwamba kutokana na mazingira ya ajali hiyo inaonyesha kuna mambo mengi yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kukomesha hali hiyo.

"Hatuwezi kuhatarisha maisha ya wananchi wetu tumepoteza watu wengi katika ajali hii, waziri mkuu atakutana na baraza la mawaziri katika mkutano ambao utahudhuriwa na wamiliki wa magari, madereva, watoa bima na idara za usalama.

"Pia watajadili hatua zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya madereva na hali ya magari yao na utoaji wa leseni na hatua zote zitachukuliwa kuhusu hali hii," alisema.

Inaelezwa kuwa katika siku za hivi karibuni ajali za barabarani katika mataifa ya Afrika zimeonekana kuongezeka, baadhi zikihusishwa na uzembe wa madereva au ubovu wa barabara.

***RFI***




Wafuasi wa Rais wa zamani wa Brazil, Jair Bolsonaro, wakikabiliana na polisi katika maandamano nje ya Ikulu, mjini Brazilia jana**. PICHA: REUTERS**

# Upinzani waruhusiwa kushiriki uchaguzi Benin

**PORTO-Novo, Benin**

WAGOMBEA wa upinzani wameruhusiwa kugombea katika uchaguzi wa bunge jipya nchini Benin, ikiwa ni kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka minne chini ya utawala wa Rais Patrice Talon.

Inaelezwa kuwa uchaguzi huo uliofanyika Jumapili, ulikuwa mtihani mkubwa kwa taifa hilo la Afrika Magharibi, huku wafuasi wa Talon wakisema alileta maendeleo ya kisiasa na kiuchumi, wakosoaji wakieleza kuwa muhula wake ulidhoofisha demokrasia.

Waandishi wa shirika la habari la AFP walisema kuwa kulikuwa na hali ya utulivu kwenye barabara za mji mkuu wa kiuchumi, Cotonou, masoko na maduka yote yalikuwa yamefungwa.

Ilibainishwa kuwa vituo vya kupigia kura vilifungwa saa kumi alasiri kwa saa za huko, lakini muungano wa mashirika ya kiraia ulisema vituo vingi vilifunga kwa kuchelewa.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa uchaguzi wa mwisho wa bunge wa mwaka 2019 uligubikwa na machafuko mabaya, idadi kubwa ya watu ambao hawakupiga kura na kufungwa kwa mtandao wa intaneti, matukio nadra nchini Benin, ambayo awali ilipongezwa kuwa kitovu cha demokrasia eneo la Afrika Magharibi.

***VOA***

# Viongozi duniani walaani uvamizi wa majengo ya utawala Brazil

**BRASILIA, Brazil**

VIONGOZI wa mataifa kadhaa duniani wamelaani uvamizi wa majengo ya utawala nchini Brazil uliofanywa na wafuasi wa rais wa zamani wa nchi hiyo, Jair Bolsonaro ambao wanapinga matokeo ya uchaguzi mkuu uliopita.

Mkasa huo wa uliojiri mwisho wa juma lililopita, ulizusha ukosoaji mkubwa kutoka kwa viongozi wa mataifa mbalimbali yakiwamo Amerika ya Kusini, Amerika ya Kaskazini na barani Ulaya.

Wengi walielezea kufadhaishwa na vurugu iliyotokea jana mjini Brazilia, ambako wafuasi wa rais aliyeondoka madarakani nchini Brazil Bolsonaro, waliyavamia majengo ya Bunge, Mahakama ya Juu na Ikulu, kupinga utawala mpya wa mwanasiasa wa mrengo wa kushoto Rais Luiz Inacio Lula da Silva aliyeapishwa wiki moja iliyopita kuliongoza taifa hilo.

Rais Joe Biden wa Marekani alikitaja kisa hicho kuwa maudhi, akisema serikali mjini Washington inaalani vikali shambulio hilo dhidi ya demokrasia na kwamba inamuunga mkono Rais Lula.

Kiongozi wa Mexico, Andres Manuel Lopez Obrador, aliandika kupitia ukurasa wa Twitter kwamba Lula hayuko peke yake na anaungwa mkono na wana mageuzi nchini mwake nchini Mexico na eneo zima la Amerika.

Ujumbe sawa na huo ulitolewa pia na viongozi wa Argentina, Colombia, Bolivia, Cuba na Venezuela. Huku Rais wa Chile Gabriel Boric, akiutaja uvamizi huo kuwa shambulizi la woga dhidi ya demokrasia na kutumia ujumbe wake kumhakikishia Rais Lula kuwa serikali mjini Santiago inamuunga mkono kikamilifu.

Barani Ulaya, Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa alituma ujumbe wa kumuunga mkono Rais Lula na kuongeza kwamba taasisi za kidemokrasia ni lazima ziheshimiwe.

Kwa upande wa Umoja wa Ulaya (EU) kupitia mwanadiplomasia wake mkuu Joseph Borell, alisema umeshtushwa na matendo ya vurugu yaliyofanywa na waandamanaji dhidi ya majengo ya serikali mjini Brazilia na kuongeza kwamba demokrasia ya Brazil itashamiri licha ya vitimbi vya wafanya vurugu na wenye misimamo mikali.

Katika mkasa huo wa jana maelfu ya waandamanaji wanaokataa kuyatambua matokeo ya uchaguzi wa mwezi Oktoba yaliyompa ushindi Lula, walivuka vizuizi vya usalama, wakaparamia kuta za majengo na kisha kuyavamia majengo matatu ya utawala yanayopatikana eneo moja katika mji mkuu wa Brazil, Brazilia.

Pia inaelezwa kuwa Polisi walitumia mabomu ya machozi kujaribu kuwadhibiti waandamanaji ambao baadhi walitoa mwito kwa jeshi kuingilia kati ili kumrejesha Bolsonaro madarakani.

Baada ya mshike mshike wa saa kadhaa maofisa wa usalama walisema wamefanikiwa kurejesha udhibiti wa majengo hayo na mamia ya waandamanaji wamekamatwa.

Naye Rais Lula akizungumza saa chache baada ya mkasa huo aliwataja waliohusika kuwa mafashisti na aliapa kuwasaka na kuwaadhibu.

"Ninataka kuwaambia kwamba watu wote waliofanya hayo watapatikana na kuadhibiwa, watatanabahi kuwa demokrasia inatoa hakikisho la haki ya uhuru, uhuru wa mawasiliano, uhuru wa kujieleza lakini inahitaji pia watu waheshimu taasisi zilizoundwa kuimarisha demokrasia," alisema Rais Lula.

Aidha, saa chache zilizopita rais wa zamani wa Brazil Jair Bolsonaro alijitokeza kulaani kisa hicho huku akiyapinga madai yanayomhusisha kuyachochea na kwamba alitoa ujumbe huo kupitia mtandao wa Twitter muda mfupi baada ya chama chake cha Liberal Party kulaani uvamizi uliofanywa na wafuasi wake.

Chama hicho kilisema matukio yaliyoshuhudiwa mjini Brazilia yanafedhehesha, lakini hayawakilishi mtazamo wa Chama cha LP wala Bolsonaro na kwamba chama hicho kinaheshimu demokrasia.

***DW***

# KAZADI AWATISHA MAYELE, PHIRI

**Na Saada Akida, Zanzibar**

BAADA ya kuonyesha kiwango kizuri katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, mshambuliaji mpya wa Singida Big Stars, Kazadi Kasengu, amesema amekuja kuleta upinzani katika idara ya kufumania nyavu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika mbio za ufungaji bora kwenye Ligi Kuu Bara, kwa sasa zinaongozwa na Fiston Mayele (Yanga SC) mabao 14 akifuatiwa na Moses Phiri aliyecheka na nyavu mara 10 na John Bocco (Simba) mwenye mabao tisa.

Wachezaji wengine wanaoonyesha kasi katika mbio hizo ni Sixtus Sabilo (Mbeya City) mwenye mabao saba huku Reliant Lusajo (Namungo FC), Idris Mbombo (Azam FC), Feisal Salum (Yanga) na Saido Ntibanzokiza (Simba), kila mmoja akifumania nyavu mara sita hadi sasa ligi hiyo ikiwa katika raundi ya 19.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kazadi alisema anafurahi kupata nafasi ya kucheza soka Tanzania Bara na anafahamu upinzani mkubwa ulioko kati ya timu hadi nafasi ya ufungaji na kwamba anamheshimu Mayele katika katika ufumaniaji nyavu.

Alisema amemfuatilia Mayele ambaye anaongoza mbio hizo na kwamba lengo lake ni kuja kuleta upinzani katika kufumania nyavu ili kufikia malengo anayoyatarajiwa kuyatekeleza katika Ligi Kuu Bara.

"Kufunga kwangu ni jambo la kawaida nina imani nitaleta upinzani mkubwa katika Ligi ya Tanzania, kuhusu Mayele ni kaka yangu, naheshimu uwezo wake, kubwa nimekuja Tanzania kufanya kazi na kutoa upinzani kwa washambuliaji wa Ligi Kuu," alisema Kazadi aliyewaondoa Azam FC katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi juzi.

Alisema katika maisha yake ya soka amewahi kufunga hat-trick mara moja akiwa kwao nchini Congo na kuhusu kufunga mabao manne katika mechi moja ni mara ya kwanza katika mchezo wa juzi wa Kombe la Mapinduzi dhidi ya Azam FC.

Kazadi amesaini mkataba wa miaka mitatu kuitumikia Singida Big Stars na tayari ameshaifungia mabao matano katika michezo mitatu ya Kombe la Mapinduzi inayoendelea visiwani Zanzibar na kuipeleka timu yake fainali.

Singida Big Stars imetinga fainali baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Azam FC katika nusu fainali ya kwanza iliyopigwa juzi Uwanja wa Amaan, Zanzibar mabao yote yakifungwa na Kazadi huku ikiwa ni hat-trick ya kwanza katika mashindano hayo msimu huu yaliyoanza rasmi Januari Mosi, mwaka huu.

Kazadi anakuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 4-0 katika mechi moja kwenye historia ya michuano hiyo tangu mwaka 2015, wachezaji wengi wameishia kupiga hat-trick akiwamo Simon Msuva wakati akiitumikia Yanga dhidi ya Taifa ya Jang'ombe mwaka 2017 na Abdulswamad Kassim (Hazgut) akiitumia Jang'ombe Boys dhidi ya KVZ.

Singida Big Stars sasa itacheza fainali Ijumaa wiki hii dhidi ya mshindi wa nusu fainali ya pili kati ya Namungo FC na Mlandege FC iliyopigwa jana usiku katika Uwanja wa Amaan.

## 'BALL ITEMBEE'..




Makocha wa Simba, Kocha Mkuu Robertinho Oliveira (kulia) na msaidizi wake, Juma Mgunda, wakiteta jambo baada ya kumalizika mechi ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya KVZ na kushinda bao 1-0. Kwa sasa timu hiyo iko Dubai, Falme za Kiarabu ikijiandaa kwa mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

# KMC bila nyota saba kuivaa Mtibwa Sugar

**Na Hadija Mngwai**

WAKATI KMC FC ikianza kujiwinda rasmi na mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar utakaopigwa Uwanja wa Manungu Complex Ijumaa wiki hii, itawakosa nyota wake saba katika mechi hiyo, imeelezwa.

KMC ambayo ipo nafasi ya tisa ya msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 22, mbili nyuma ya Mtibwa Sugar inayoshika nafasi ya nane, itacheza mechi hiyo ikitoka kupoteza mchezo uliopita dhidi ya Ihefu FC. Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, alisema kikosi chao kimerejea kambini tangu jana, tayari kikijiwinda na mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar ugenini, lakini kinakabiliwa na kuwakosa nyota saba kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo majeruhi.

"Kikosi cha KMC kimerejea kambini leo (jana), kuendelea na maandalizi dhidi ya Mtibwa Sugar tutakaocheza Januari 13 tukiwa ugenini.

"Mchezo utakuwa mgumu kwetu kutokana na kuwakosa wachezaji wetu saba akiwamo Sadalah Lipangile, Ibrahimu Ame, Matheo Anton, Steve Nzingamasobo na Ismail Gambo ambao watakosekana kutokana na changamoto za kifamilia pia wachezaji wetu Emmanuel Mvuyekure na Hance Masoud hawa ni majeruhi wa muda mrefu.

"Pia kocha wetu Thierry Hitimana, aliyekuwa Rwanda kwenye msiba wa mdogo wake, amerejea leo (jana) na tayari ameshaanza kukinoa kikosi chake kwa lengo la kuhakikisha tunafanya vizuri katika mechi zilizobakia za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara ili tumalize katika nafasi nzuri kwenye msimamo," alisema Mwagala.

## Nchimbi aibukia Fountain Gate

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Yanga na Timu ya Taifa, Taifa Stars, Ditram Nchimbi, amejiunga na Klabu ya Fountain Gate inayoshiriki Ligi ya Championship kwa mkataba wa miezi sita.

Mshambuliaji huyo amejiunga na timu hiyo inayoshika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo akiwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na Klabu ya Yanga.

Kabla ya kuwa huru, Yanga ilimpeleka mchezaji huyo Klabu ya Geita Gold kwa mkopo na ulipomalizika akawa hana timu.

"Kweli nimesaini mkataba wa miezi sita na Fountain Gate, walinifuata na kunishawishi na mimi nilikubali siyo kwa sababu ya pesa bali na mipango yao pia.

"Kulikuwa na timu nyingi za ligi ambazo zilionyesha nia ya kunihitaji, lakini kama mimi niliangalia wapi walipo, nikaona ni bora tu nije kwenye timu ambayo unaweza kucheza na kuipandisha daraja na kwenda Ligi Kuu, kuliko kwenda timu ambayo unakwenda kucheza halafu mnashuka daraja," alisema Nchimbi ambaye kuna wakati alikuwa tegemeo kwenye kikosi cha Yanga.

## Geita Gold yafunguka wachezaji wake kutimka

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Geita Gold imeibuka na kusema kuwa haikimbiwi na wachezaji wake kama baadhi ya watu wanavyodhani bali wanauza na kupata pesa kitu ambacho ni kawaida kwa maisha ya mpira wa miguu.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Leonard Bugomola, amesema hayo jana kutokana na mfululizo wa kutimka kwa wachezaji wa timu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo kwenda kwenye klabu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Jumla ya wachezaji watano wameshatimka kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo, akiwamo Kelvin Nashon ambaye juzi alitangazwa kuwa ni mchezaji wa Singida Big Stars.

"Hakuna mchezaji aliyetukimbia, wote wamenunuliwa na klabu imepata pesa, hii inaonyesha kuwa tuna wachezaji wazuri, wametoka kufanya vizuri hapa na hata huko wanakowenda wanaendelea kufanya vema kama vile Saido Ntibazonkiza, ametoka hapa lakini angalia ambacho amekifanya akiwa Simba mechi ya kwanza tu, hata Yusuph Kagoma unaona anachokifanya huko Namungo, kwa hiyo tuna wachezaji wazuri ambao wanatamaniwa na klabu zingine na kuuza wachezaji na kusajili wengine ni jambo la kawaida tu kwenye maisha ya mpira wa miguu,' alisema mwenyekiti huyo.

## ZISIKUPITE

### BALDE ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal ina nia ya kumsajili nyota wa Barcelona, Alejandro Balde, huku beki huyo wa pembeni wa Hispania mwenye umri wa miaka 19, akiwa bado hajasaini mkataba mpya na klabu yake. ***(Sport)***

### DIABY AWANIA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inajiandaa kumnunua mshambuliaji wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 23 huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23 akihusishwa kwa muda mrefu kutaka kuhamia Ligi Kuu England. ***(Bild)***

### MORENO KUTUA VILLA
ASTON Villa wanaaminika kukaribia kufanikiwa katika mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Hispania, Alex Moreno, kutoka Real Betis mwenye umri wa miaka 29. ***(Football Insider)***

### GARNACHO ATAKIWA MADRID
KLABU ya Atletico Madrid inataka kumsajili tena kinda aliyewahi kuchezea timu zao za vijana, Alejandro Garnacho, kutoka Manchester United, lakini klabu hiyo ya Old Trafford huenda ikagoma kumruhusu Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 18 kuondoka. ***(Fichajes)***

### DZEKO LULU MAN UNITED
KLABU ya Manchester United inataka kumnunua mshambuliaji wa Inter Milan na Bosnia, Edin Dzeko mwenye umri wa miaka 36, ambaye alikuwa na mafanikio makubwa awali akiwa na Manchester City. ***(Mail)***

### MAEDA ANUKIA SOUTHAMPTON
KLABU ya Southampton inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Celtic raia wa Japan, Daizen Maeda mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports)***

### SPURS KWA AMORIM, PORRO
KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, amesisitiza kuwa klabu hiyo haihofii Tottenham Hotspur kutaka kumnunua beki wa Hispania, Pedro Porro, mwenye umri wa miaka 23 na kiungo wa zamani wa Spurs, Marcus Edwards mwenye umri wa miaka 23. ***(Standard)***

### RAYA NDANI YA RADA
KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia kipa wa Brentford, David Raya mwenye umri wa miaka 27. ***(Telegraph)***

### ARTETA AMLILIA JOAO
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anashinikiza klabu hiyo kumsajili, Felix Joao katika dirisha la usajili la Januari hii. ***(Mirror)***

### ABOUBAKAR SAFI UNITED
KLABU ya Manchester United imekubali kumsajili mshambuliaji wa Cameroon, Vincent Aboubakar mwenye umri wa miaka 30 kwa mkopo kutoka Al Nassr. ***(OKAZ, via Talksport)***

### CAICEDO NA LIVER, CHELSEA
LIVERPOOL na Chelsea zinaisaka saini ya kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo, 21. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO KUTANGAZWA KOCHA MPYA WA BRAZIL

**Ninazungumza moja kwa moja, ni habari mpya, hata yeye amenialika niwe msaidizi wake...**

**SAO PAULO, Brazil**

KOCHA Mkuu wa AS Roma, Jose Mourinho, anatarajiwa kuchukua nafasi ya kuwa bosi mpya wa Brazil, kwa mujibu wa mchezaji wa zamani wa 'Selecao' hao, Carlos Alberto.

Brazil wanasaka kocha mkuu mpya baada ya Tite kujiuzulu, kama ilivyopangwa, baada ya kutolewa na Croatia katika robo fainali ya Kombe la Dunia mwezi uliopita.

Mourinho ni miongoni mwa majina ambayo yameripotiwa kujumuishwa katika nafasi hiyo, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 59, pia akitajwa kuwa huenda analengwa na Ureno kutokana na kuondoka kwa Fernando Santos, ingawa Roberto Martinez anaonekana kuwa mstari wa mbele katika kazi hiyo.

Alberto, ambaye alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya Mourinho akiwa Porto, amesema amepewa nafasi ya kufanya kazi pamoja na Mreno huyo kama sehemu ya wakufunzi wa Brazil.

"Nilikuwa nikirusha bomu hapa, lakini siwezi," alisema Alberto akiiambia Mundo GV.

"Labda (Mourinho) ni kocha wa timu ya Brazil. Ninazungumza moja kwa moja. Ni habari mpya.

"Haijalishi taarifa hizo zinatoka wapi, nakupa taarifa... maana hata yeye alinialika niwe msaidizi wake."

Mourinho aliiongoza Roma kunyakua taji la kwanza la Ligi ya Europa Conference msimu uliopita - taji la kwanza la Ulaya kwa timu hiyo ya Italia katika zaidi ya miaka 60.

Huo ulikuwa ushindi wa tano wa Mourinho Ulaya, huku kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Real Madrid, Inter, Manchester United na Tottenham Hotspur akiwa ameshinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,065,5

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 11,12 NA 13 JANUARI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/01/23 | 20:00 | AEL Limassol vs Apollon Limassol | 2.73 | 3.22 | 2.37 |
| 02. 11/01/23 | 20:00 | Kortrijk vs Mechelen | 2.62 | 3.41 | 2.44 |
| 03. 11/01/23 | 21:00 | Nantes vs Lyon | 3.22 | 3.31 | 2.19 |
| 04. 11/01/23 | 21:00 | AJ Auxerre vs Toulouse | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 05. 11/01/23 | 21:00 | AC Ajaccio vs Reims | 2.90 | 3.10 | 2.46 |
| 06. 11/01/23 | 22:00 | VVV Venlo vs Emmen | 3.05 | 3.49 | 2.17 |
| 07. 11/01/23 | 22:45 | Nottingham vs Wolverhampton | 2.63 | 3.12 | 2.68 |
| 08. 12/01/23 | 02:00 | Alebrijes De Oaxaca vs Club Celaya | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 09. 12/01/23 | 04:05 | Cancun FC vs Leones Negros Udg | 2.63 | 3.07 | 2.53 |
| 10. 12/01/23 | 18:00 | Ghazl EL Mahallah vs Enppi Club | 2.65 | 2.65 | 3.15 |
| 11. 12/01/23 | 20:45 | Heracles Almelo vs GO Ahead Eagles | 2.21 | 3.51 | 2.96 |
| 12. 12/01/23 | 22:45 | Union Saint Gilloise vs KAA Gent | 2.24 | 3.45 | 3.10 |
| 13. 13/01/23 | 11:45 | Macarthur FC vs Central Coast Mariners | 2.47 | 3.28 | 2.74 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: BARCA INA NAFASI KUTWAA TAJI LA LALIGA



**BARCELONA, Hispania**

XAVI amesema walipata "pointi tatu za dhahabu" kutoka kwa Atletico Madrid na kuipa Barcelona "ari na kujiamini" katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Ousmane Dembele alifunga bao pekee katika mchezo huo kwenye Uwanja wa Civitas Metropolitano Jumapili na kuifanya Barca kuwa mbele kwa pointi tatu kileleni dhidi ya Real Madrid.

'Blaugrana' hao walikuwa na wakati mzuri hasa baada ya Real Madrid kukutana na kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Villarreal, Jumamosi.

Barca walikuwa wamefungwa na Espanyol katika mchezo wao wa kwanza wa LaLiga baada ya Kombe la Dunia, hivyo Xavi alijua umuhimu wa kukifunga kikosi cha Diego Simeone.

Alisema: "Ni ushindi, lakini si pointi tatu pekee, inatupa ari kubwa na kujiamini kwa muda uliosalia wa ligi.

"Tuna uwezo wa kushinda katika uwanja mgumu kama huu. Bila kucheza vizuri kama tulivyocheza dhidi ya Espanyol, leo (juzi) tumejua jinsi ya kuteseka na tukachukua pointi tatu za dhahabu."

Xavi aliongeza: "Pointi tatu za dhahabu. Tumetumia nafasi yetu. Wamesisitiza na tunajua jinsi ya kuteseka.

"Na jinsi ilivyo muhimu kuweka bao safi. Kama nilivyosema kwenye mchezo wa Espanyol kwamba tulistahili zaidi, leo labda bila kucheza vizuri tumepata pointi tatu."

# Mbappe amshukia Le Graet kisa Zidane

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amemshutumu Noel Le Graet kwa kutomheshimu Zinedine Zidane baada ya jibu la rais huyo wa Shirikisho la Soka la Ufaransa kukataa mapendekezo ya kocha huyo wa zamani wa Real Madrid kujiunga na Brazil.

Jumamosi ilitangazwa kwamba, Didier Deschamps ametia saini mkataba mpya wa miaka minne kama kocha mkuu wa Ufaransa na kumruhusu kuinoa 'Les Bleus' kwenye Kombe la Dunia la nne mwaka 2026.


Nyota wa zamani wa Ufaransa Zidane alikuwa akihusishwa na kazi ya juu ya nchi yake mara kadhaa, ikiwa ni pamoja na baada ya kushindwa kwao katika fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Argentina mwezi uliopita.

Hata hivyo, huku nafasi hiyo ikitarajiwa kukaliwa kwa siku za usoni, Zidane alipendekezwa kumrithi Tite kama kocha mkuu wa Brazil.

Alipoulizwa kuhusu uvumi unaomhusisha Zidane na 'Selecao' Jumapili, Le Graet aliiambia RMC kwamba "wala sifikirii" na kuongeza kuwa hata kama angempigia simu mshindi huyo wa Kombe la Dunia 1998 asingejibu simu yake.

Maoni hayo yalivutia ukosoaji kutoka kwa mchezaji nyota Mbappe, ambaye aliandika kwenye Twitter: "Zidane ni Ufaransa, hatumdharau gwiji huyu.

Zidane amekuwa hana kazi tangu alipoondoka Madrid mwaka 2021, akiwa ameiongoza 'Los Blancos' kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu na mataji mawili ya LaLiga.



505,647/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/01/23 | 18:00 | Nottingham Forest vs Leicester City | 2.80 | 3.30 | 2.46 |
| 02. 14/01/23 | 18:00 | Wolverhampton Wanderers vs West Ham United | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 03. 14/01/23 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich Albion | 2.95 | 3.20 | 2.40 |
| 04. 14/01/23 | 18:00 | Preston North End vs Norwich City | 2.95 | 3.25 | 2.38 |
| 05. 14/01/23 | 18:00 | Reading FC vs Queens Park Rangers | 2.46 | 3.25 | 2.80 |
| 06. 14/01/23 | 18:00 | Sunderland AFC vs Swansea City | 2.49 | 3.25 | 2.75 |
| 07. 14/01/23 | 18:00 | DR Congo vs Uganda | 2.39 | 2.75 | 3.45 |
| 08. 14/01/23 | 18:15 | Girona FC vs Sevilla FC | 2.40 | 3.25 | 2.90 |
| 09. 14/01/23 | 20:15 | KAS Eupen vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.35 | 2.42 |
| 10. 14/01/23 | 20:45 | FC Volendam vs RKC Waalwijk | 2.65 | 3.50 | 2.46 |
| 11. 14/01/23 | 21:00 | Ivory Coast vs Senegal | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 12. 14/01/23 | 23:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.15 | 2.80 |
| 13. 15/01/23 | 16:00 | Getafe CF vs Espanyol Barcelona | 2.50 | 2.95 | 2.95 |
| 14. 15/01/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs FC Utrecht | 2.80 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 15/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs Clermont Foot 63 | 2.42 | 3.40 | 2.75 |
| 16. 15/01/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs FC Nantes | 2.45 | 3.40 | 2.70 |
| 17. 15/01/23 | 17:00 | Stade Reims vs OGC Nice | 2.55 | 3.20 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 10/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5964 | Perth Glory vs Brisbane Roar | 2.79 | 3.29 | 2.42 |
| 15:20 | 4807 | Alshoulla vs AL Riyadh | 2.81 | 2.81 | 2.57 |
| 15:30 | 2773 | Thailand vs Malaysia | 1.41 | 4.11 | 6.84 |
| 16:15 | 3007 | United Arab Emirates vs Kuwait | 1.78 | 2.99 | 4.90 |
| 17:40 | 3775 | Al Qadisiyah vs Al Ahli Jeddah | 3.89 | 2.92 | 2.00 |
| 19:15 | 3674 | Qatar vs Bahrain | 3.03 | 2.78 | 2.44 |
| 20:30 | 2324 | Al Raed Club vs Al Hilal Riyadh | 5.80 | 4.60 | 1.47 |
| 20:30 | 4861 | Mamelodi Sundowns vs Chippa Utd | 1.37 | 4.25 | 8.51 |
| 20:45 | 3891 | Twente vs Telstar | 1.25 | 5.45 | 8.37 |
| 21:45 | 5933 | Leixoes vs Famalicao | 3.07 | 3.17 | 2.18 |
| 22:00 | 1985 | NAC Breda vs FC Eindhoven | 2.23 | 3.36 | 2.82 |
| 22:00 | 3878 | Lincoln vs Accrington | 2.09 | 3.31 | 3.12 |
| 22:30 | 1755 | Wrexham vs Bromley | 1.31 | 5.11 | 8.06 |
| 22:45 | 1349 | Farnborough Town vs Slough Town | 1.64 | 3.79 | 4.38 |
| 22:45 | 1528 | Wealdstone vs Chesterfield | 4.14 | 3.65 | 1.76 |
| 22:45 | 1558 | Valenciennes vs Annecy FC | 2.22 | 3.02 | 3.36 |
| 22:45 | 1826 | Glenavon vs Crusaders Belfast | 3.36 | 3.56 | 1.92 |
| 22:45 | 1864 | Aldershot vs Dagenham and Redbridge | 2.56 | 3.39 | 2.51 |
| 22:45 | 2058 | Le Havre vs Sochaux | 2.22 | 3.02 | 3.36 |
| 22:45 | 2138 | Whitby Town vs Guiseley | 2.35 | 3.50 | 2.57 |
| 22:45 | 2215 | Rodez Aveyron vs Niort | 2.34 | 2.97 | 3.16 |
| 22:45 | 2689 | Nimes vs Metz | 2.97 | 3.12 | 2.37 |
| 22:45 | 3156 | Dover vs Taunton Town | 2.22 | 3.25 | 2.91 |
| 22:45 | 3703 | Cliftonville Belfast vs Linfield Belfast | 2.95 | 3.20 | 2.23 |
| 22:45 | 3774 | Matlock Town vs Marine FC | 2.35 | 3.50 | 2.57 |
| 22:45 | 3788 | Flint Town United vs The New Saints | 14.51 | 7.16 | 1.12 |
| 22:45 | 4069 | Newry City AFC vs Coleraine FC | 5.45 | 3.89 | 1.52 |
| 22:45 | 4123 | Notts County vs Boreham Wood | 1.31 | 5.11 | 8.06 |
| 22:45 | 4258 | Amiens vs Guingamp | 2.26 | 3.12 | 3.17 |
| 22:45 | 4616 | Bradford City vs Rochdale | 1.77 | 3.56 | 4.26 |
| 22:45 | 4655 | Buxton FC vs Chorley | 2.76 | 3.30 | 2.30 |
| 22:45 | 4769 | St Etienne vs Laval | 1.95 | 3.32 | 3.76 |
| 22:45 | 4892 | Glentoran Belfast vs Ballymena Utd | 1.30 | 4.88 | 8.00 |
| 22:45 | 4921 | PAU FC vs Grenoble Foot | 2.40 | 3.01 | 3.01 |
| 22:45 | 5002 | Bala Town vs Gap Connahs Quay | 2.34 | 3.21 | 2.77 |
| 22:45 | 5019 | Paris FC vs Dijon | 2.13 | 3.03 | 3.58 |
| 22:45 | 5028 | Bolton vs Portsmouth | 2.10 | 3.31 | 3.11 |
| 22:45 | 5064 | Bristol Rovers vs Plymouth | 2.53 | 3.41 | 2.43 |
| 22:45 | 5208 | Corinthian Casuals vs Horsham | 3.74 | 3.89 | 1.74 |
| 22:45 | 5246 | US Quevilly Rouen vs Bastia | 2.39 | 3.07 | 2.97 |
| 22:45 | 5638 | Leiston vs Coalville Town | 2.17 | 3.79 | 2.67 |
| 22:45 | 5725 | Cheltenham vs Salford City | 2.18 | 3.35 | 2.92 |
| 22:45 | 5881 | AFC Fylde vs Blyth Spartans | 1.54 | 3.98 | 5.05 |
| 22:45 | 5882 | Caen vs Bordeaux | 2.39 | 3.02 | 3.02 |
| 23:00 | 3051 | Newcastle vs Leicester | 1.63 | 3.87 | 4.96 |
| 23:00 | 3681 | Aberystwyth Town vs Penybont | 4.88 | 4.00 | 1.55 |
| 23:00 | 3928 | Sparta Rotterdam vs PSV Eindhoven | 5.45 | 4.09 | 1.49 |
| 23:00 | 4943 | Manchester Utd vs Charlton | 1.16 | 7.25 | 13.82 |
| 23:00 | 5644 | Inter vs Parma | 1.20 | 6.73 | 10.89 |
| 23:45 | 2471 | Varzim vs Benfica | 8.37 | 5.26 | 1.27 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# AZAM FC YAKIRI MAJI YA SHINGO SINGIDA BIG STARS

**Na Saada Akida, Zanzibar**

KAIMU Kocha Msaidizi wa Azam FC, Kalimangonga Ongala, amekiri kuzidiwa na Singida Big Stars kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi juzi usiku na kwamba haikuwa bahati yao kucheza fainali mwaka huu.

Azam FC imeondolewa katika mashindano hayo baada ya kukubali kichapo cha mabao 4-0 dhidi ya Singida Big Stars katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Amaan, visiwani hapo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kalimangonga alisema walizidiwa katika nafasi nyingi na Singida Big Stars walistahili kupata ushindi kwa sababu safu yake ya ulinzi alipoteza umakini na kuruhusu mabao hayo manne.

Alisema hakuna wa kumlaumu katika matokeo ya mchezo wa juzi na wameona mapungufu ya kikosi chao hivyo wanaenda kuyafanyia kazi kabla ya kurejea kwa raundi ya 20 ya Ligi Kuu mwishoni mwa wiki hii.

"Ni kweli mchezo wa leo tumezidiwa kiufundi, wenzetu walikuwa bora katika kila eneo, kulingana na kiwango walichokionyesha walistahili ushindi ni wapongeze, lakini tunarudi nyumbani kwa ajili ya kuimarisha kikosi kwa kufanyia kazi madhaifu yetu," alisema Kalimangonga.

Kuhusu makosa yaliyofanywa na kipa, alisema kabla ya kumtupia lawama nyanda huyo walishindwa kucheza mchezo wao kwa kufanya makosa na kusababisha kuadhibiwa kwa idadi hiyo kubwa ya mabao.

Kocha huyo alisema baada ya kuondolewa katika michuano hiyo sasa wanarejea Dar es Salaam kujipanga kwa michezo yao ya raundi ya 20 ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuhakikisha wanafanya vizuri na kumaliza katika nafasi tatu za juu.

Juzi Azam FC ilimtambulisha kipa mpya kutoka nchini Ghana, Abdulai Iddrisu, kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Bechem United ya Ghana, ambaye jana asubuhi alidaka katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Polisi Zanzibar.




Kali Ongala

# SIMBA KUJIPIMA NA TIMU YA ULAYA

INATOKA UK. 24

sha kikosi kilichokwenda huko.

Kocha Robertinho amesema yeye kama kocha anachohitaji ni wachezaji wenye vipaji na uzoefu ili kutengeneza kikosi cha ushindi na cha kuogopesha.

Hata hivyo, alisema hayo yote hayawezi kufanyika kama hakutokuwa na ushirikiano kati yao.

"Ili kufanya yote hayo, kunahitajika ushirikiano kati ya wachezaji wenyewe, makocha na benchi la ufundi, unajua mimi nikiwaheshimu wachezaji wangu nao wataniheshimu pia. Mfano nikwambie tu, Juma Mgunda ni rafiki yangu sana, kila muda niko naye kwa sabahu ana uzoefu na soka la Kiafrika na ni kaka yangu pia," alisema kocha huyo aliyetokea klabu ya Vipers ya Uganda.

Michezo
Jumanne Januari 10, 2023
Nipashe



UKURASA 21

**Mourinho kutangazwa kocha mpya wa Brazil**

# MUSONDA, YANGA SASA KIMEELEWEKA

## ●●●Kufunga usajili wa Jangwani, huku akitarajiwa kuibua vita vya namba na Mayele ambaye…

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikiendelea na mazoezi ya kujiandaa na raundi ya 20 ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu FC, uongozi wa timu hiyo umefanikiwa kunasa saini ya mshambuliaji wa Power Dynamos ya Zambia, Kennedy Musonda, ambaye anatua kupambania namba na kinara wao wa ufungaji, Fiston Mayele, imefahamika.

Kikosi cha timu hiyo kinaendelea kujinoa katika kambi yao ya siku zote pale Avic Town, Kigamboni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Ihefu FC utakaopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatatu ijayo.

Katika dirisha hili dogo, Yanga tayari imeshasajili na kutambulisha mchezaji mmoja tu, Mudathir Yahya na muda wowote kuanzia sasa watamtambulisha Musonda ambaye gazeti hili limepata taarifa kuwa mshambuliaji huyo amesaini mkataba wa miaka miwili.

Kwa mujibu wa chanzo cha uhakika ndani ya klabu hiyo, kimeeleza kuwa wiki iliyopita Meneja wa nyota huyo, George Deddah, alikuwapo hapa nchini kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kimkataba na kukubaliana asaini miaka miwili kuitumikia klabu hiyo.

Deddah ambaye yuko visiwani Zanzibar alisema yuko nchini kwa ajili ya mazungumzo na baadhi ya klabu ambazo zimeonyesha nia ya kuwasajili wachezaji wake akiwamo Musonda.

"Niko hapa nchini kufuatilia [masuala] ya baadhi ya wachezaji wangu, kuhusu Musonda ni kweli kuna baadhi ya timu zina muhitaji, lakini kwa sasa sitaweka wazi hadi hapo itakapomtambulisha rasmi," alisema Deddah.

Kwa upande wa Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, alisema ndani ya wiki hii kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili watatangaza majina makubwa ya wachezaji wawili ambao wako hatua ya mwisho ya mazungumzo.

**"Kabla ya kufugwa kwa dirisha la usajili, tutashusha majina mawili mapya mazito, usajili tunaoufanya ni mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha wetu, Nasreddine Nabi kwa kutuhitaji kusajili kulingana na maeneo aliyoyataja mshambuliaji wa kati na beki ya kati.**

"Kama nilivyosema awali, mchakato unaendelea na mazungumzo yako katika hatua nzuri na muda wowote ndani ya hizi siku 10 tutatangaza majina ya wachezaji hao na kufunga usajili wetu," alisema Arafat.

Alisema usajili unaofanywa ni kwa ajili kuziba madhaifu waliyoyabaini kwa kujiimarisha kuwa bora zaidi hasa katika safu ya ushambuliaji ambayo kwa sasa inaongozwa na kinara wa mabao, Mayele.



Kennedy Musonda

## Simba kujipima na timu ya Ulaya

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

WAKATI ikiwa kwenye siku ya tatu ya mazoezi yake Dubai, huenda timu hiyo ikacheza mechi moja na timu kutoka barani Ulaya, taarifa kutoka ndani ya kambi yao ya mazoezi zimeeleza jana kuwa mabosi wa klabu hiyo kwa sasa wanahangaika kufanikisha hilo na mambo yakikaa sawa wataliweka hadharani.

Straika Mosses Phiri naye ameungana na kikosi hicho akitokea nchini Zambia, huku kiungo mkabaji Clatous Chama akitarajiwa kutua leo, wakati huu Kocha Mkuu, Mbrazil Robertinho Oliveira, akitaka ushirikiano baina ya wachezaji wenyewe, makocha na benchi zima la ufundi ili kutengeneza kikosi chenye mafanikio.

"Kwa sasa viongozi wapo kwenye harakati za kufanikisha mchakato huo, huenda tukacheza na timu kutoka Ulaya kama mambo yatakwenda vizuri, lakini hata mimi mwenyewe sijui ni nchi gani, au inatoka Ulaya gani, Magharibi au Mashariki, viongozi wakikamilisha hilo tutalitangaza, lakini ni moja kati ya timu za huko na mechi za kirafiki zitakuwa mbili, nyingine tutacheza na timu ya hapa hapa Dubai," kilisema chanzo hicho.

Wakati timu hiyo ikiondoka Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, alibainisha kuwa timu hiyo itacheza mechi mbili za kirafiki ikiwa Dubai ingawa hakuzitaja.

Mchezaji majeruhi wa muda mrefu wa timu hiyo, Peter Banda ameanza rasmi mazoezi, huku akipewa mazoezi maalum ili kurejesha utimamu wa mwili.

Video iliyotolewa na mtandao wa kijamii wa klabu hiyo ambayo ilikuwa ikioonyesha jinsi wachezaji wa timu hiyo wakifanya mazoezi, ilimwonyesha pia Banda ambaye aliumia kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara Novemba 9, mwaka jana kwenye mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Singida Big Stars akifanyiwa mazoezi ya peke yake.

Taarifa kutoka Dubai zinasema kuwa straika Phiri ambaye aliumia Desemba 21, mwaka jana kwenye mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Kagera Sugar uliochezwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, amewasili akitokea moja kwa moja kwao Zambia, huku Chama akitarajiwa kutua leo kukamili-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >